# *USHUHUDA BAHARINI*

Hebu na tuendelee tu kusimama, usiku wa leo, kwa muda kidogo, na hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi, mbele za Bwana wetu. Sijui, usiku wa leo, wakati tumeinamisha vichwa vyetu sasa, kama tuna haja zozote ambazo—ambazo bado hazijajibiwa, nanyi mnataka Bwana azijibu, usiku wa leo, inua mkono wako, kama ukipenda. Na tuombe.

2 Baba yetu Mtakatifu, tunakujia Wewe, usiku wa leo, katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu Kristo, tukija kwa mwaliko Wake kwenye Kiti kikuu cha Enzi cha Milele cha rehema ya Mungu. Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utatujalia haja tunazoombea. Sasa, Baba, kila mmoja anafanya haja yake ijulikane Kwako kwa njia yao, nami nitakujulisha yangu, Mungu, upate kujibu kila moja ya haja zao, hiyo ndiyo yangu. Nami naweka maombi yangu, pamoja na yao, juu ya Sadaka ambapo Dhabihu yetu imewekwa Pale. Na, katika Jina la Yesu Kristo, jibu usiku wa leo, Bwana, Tupe ridhaa yote ya imani kwamba tunapokea tuombayo. Waokoe waliopotea, wape furaha wanaosafiri, wakingojea Kuja kwa Bwana, waponye wagonjwa na wanaoteseka, pokea utukufu na heshima kwa Jina Lako. Sasa, pamoja na maombi yetu, na pamoja na kusomwa kwa Neno, na sisi wenyewe, tunajikabidhi Kwako, tuko mikononi Mwako, tutumie upendavyo.

3 Baba, tunajua ya kwamba kuna watu wengi ambao hawataisoma Biblia, lakini umelifanya Kanisa Lako nyaraka zilizoandikwa, Neno la Mungu lililodhihirishwa. Nao watu wanaweza kuyatazama maisha, na kuona kile Neno la Mungu lilicho, kwa maana maisha ya Mkristo hudhihirisha Neno. Basi tunapaswa kuwa Wakristo wa aina gani, Bwana? Tusaidie kuwa Wakristo wa Biblia, ili kazi na Maisha ya Yesu Kristo yajulikane kupitia sisi. Katika Jina Lake, tunaomba. Amina.

4 Mwaweza kuketi. Ni majaliwa makubwa jinsi gani kuwa na siku hizi tatu usiku pamoja nanyi watu! Ninataka kumshukuru, kwanza, Ndugu Eddie, kwa kunialika hapa, na kwa kuwaleta hawa ndugu wengine wazuri hapa waje kusaidia, wanamuziki, na—na yule dada aliyecheza piano, na—na ndugu na dada walioimba, mlifikiri sikuusikia, lakini niliusikia, nilikuwa nimeketi tu pale kwenye gari baada ya kufika huku, nami nikausikia huo uimbaji, kwa marafiki wetu wa Kihindi waliotuimbia, na—na yule jamaa mdogo aliyeimba wimbo huu maalum. Nami ninataka kupata kanda ya huo kwa matumizi yangu mwenyewe, nautaka huo. Nami nina kanda za watu ulimwenguni kote wakiimba, nami ninataka kuwanasa marafiki zangu Wahindi kwenye kanda wakiimba.

5 Tunawashukuru kila mmoja, na kwa yule muungwana aliyeturuhusu kuuchukua ukumbi huu, nasi tu—tunawashukuru sana. Nami naamini kwamba—kwamba hii itakuwa . . . Siku tatu usiku ulikuwa tu ni kitu kama njia ya utangulizi, kufahamiana nanyi. Nami natumaini kurudi siku moja, Bwana akipenda nanyi mnataka nirudi, ili tuweze kukaa muda mrefu.

6 Nilikuwa na majaliwa alasiri hii ya kuteremka kwenye hifadhi yenu, huko chini mtoni, nadhani wanaiita, ghuba ndogo, rasi, huko chini hadi mahali hifadhi ilipokuwa, na pamoja na ndugu, ndugu Mkristo, katika mashua yake. Tulivua samaki kisha tukarudi. Nilipata kuwaona baadhi ya ndugu, huko ziwani, ama, baharini, kwenye mashua zao wakivua samaki. Ndipo nikawazia, nilipokuwa huko nje, "Laiti ningekuwa na wakati usiku wa leo kuhubiri mahubiri, 'Bwana, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha tusipate kitu, lakini hata hivyo, kwa neno Lako tutaushusha wavu.'" Tuutupe upande huo mwingine wa mashua. Lakini, nikizungumza na ndugu huyu, ambaye mwenyewe ni Mhindi, naye anaamini kuwa ingekuwa sawa, labda nitakaporudi, kushuka tu kwenye hifadhi, na kuishi huko kwa muda kidogo, kutoka mahali hadi mahali miongoni mwa watu, na—na kuzungumza nao, na kuomba pamoja nao huko. Ninyi . . .

7 Kwa kweli, ni . . . inaudhulumu mkutano kuufanya kama tunavyofanya hapa, kuingia tu haraka, nawe unalitazama, na kushangaa, na [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] huyo umeondoka. Mnaona? Nami niliketi chini, na kulielezea, leo, kwa ndugu huyu Mhindi. Nami tayari nimelisahau jina lake. (Lilikuwa ni nani . . . ?) Ndugu Johns- . . . [Ndugu mmoja anasema, "Robert Johnson."] Robert Johnson. Anaweza kuwazungumzia na kuwaelezea mengine mengi kuhusu hilo; tuliketi ndani ya teksi. Basi nilipokuwa nikimwelezea, nilisema, "Ndugu Robert . . . " kitu fulani tulichopaswa kuomba. Naye alikuwa akiniambia jinsi Bwana alivyokuwa amejibu maombi, na kumpa mvulana wake mdogo, kadhalika, jinsi mkewe alivyoingia katika Roho wa Mungu, na kunena kwa lugha, na kunena kwa lugha yake, yeye na mkewe wakiwa wa kabila tofauti, na jinsi ambavyo—ambavyo Mungu alikuwa amewabariki, na yote. Halafu basi nikasema, "Sasa, tutamwomba Bwana jambo fulani." Nami nikasema, "Ndipo katika hili, Ndugu Robert, ndipo utajua kuwaambia watu." Ndipo tulipomwomba Bwana, huyu hapa akaja moja kwa moja na kulifunua.

8 Na papo hapo, ile mashua ikatikisika kote, nami nikasema, "Kwani ulifikiri tuligonga gogo?" Naye akanitazama. Nikasema, "La, hiyo ilikuwa ni Yeye akitujulisha. Unaona?" Nasi tukaangalia kote nyuma, hapakuwapo na magogo wala chochote kile kilichowekwa pale kuigonga, ilikuwa moja kwa moja huko mbali baharini. Kwa hivyo mnaona, "walipokwisha kuomba,

mahali pale walipokusanyika pakatikisika," mnaona. Naye atalikumbuka daima, na mimi pia, Uwepo wa Bwana, wakati hao wengine wote wamejinyoosha kwenye sitaha wamelala usingizi. Kwa hiyo, tulikuwa na ushirika mdogo pamoja. Nami natumai kurudi tena.

9 Ha—hamnijui kabisa, nanyi mna haki ya kushuku kidogo, ila ninashukuru hamnishuku. Labda wengine watashuku. Lakini nilifikiri labda. . .Nimetazamia ambapo ningemwona Bwana akifanya jambo la ajabu sana ambalo lingewafanya hao wengine, kule chini, kuona kilichokuwa kimetukia. Na kwa hiyo ninatumaini. Nami niliambiwa kwamba jambo fulani lilitukia mkutanoni, nami nikamwambia Ndugu Robert la kumwambia m—mzazi wa huyo mtu, na hivyo, jinsi ya kuendelea ikiwa Shetani atajaribu kurudi. Kwa hiyo sasa . . .

10 Nami ninataka kuwashukuru wazungu kwa ushirikiano wenu mzuri, kuja hapa ndani kuninii. . .pamoja na ndugu zenu Wahindi na hao, na kusimama pamoja, na kusaidia kuufadhili, kuweka mabega yenu—yenu nyuma ya gu—gurudumu, kama tusemavyo, na kusukuma kwa nguvu zenu zote. Naye Mungu amewainua pia, kwa sababu kuna wengi wa Roho. . .mara nyingi Roho wa Mungu hutoka nje. . .alitoka akapitia mkutanoni mle na kuwashika hao, na kuwaponya. Na—nami ninataka kuwashukuru, ninyi ni wema sana. Mungu awabariki daima.

11 Na sasa, ama kesho usiku, tuko huko Victoria. Nadhani wamelitangaza, mahali ulipo, ambapo mkutano utakuwa, kama baadhi yenu mna marafiki mle, mbona, wapigieni simu walio wagonjwa, tungefurahia kuja. Sasa, kile ambacho ningetaka kufanya nitakaporudi ingekuwa ni kuchukua muda mrefu tu, mnaona, bila kujaribu kukaa muda mrefu sana usiku, lakini labda basi kufanya i—ibada ya asubuhi kwa mafundisho na kuwaambia vile adui atakavyofanya. Na kuwaacha wale ambao adui ameondolewa kwao, kisha akarudi. . .Tunaona wakati pepo mchafu amemtoka mtu, anatembea mahali pakavu, kisha anarudi tena pamoja na pepo wengine saba. Nao watu wengi wanafikiri kwamba wakati mwingine kwa sababu waliugua, kwamba hiyo ni ishara, vema. . .Hebu tuchukue kwa mfano, muda kidogo tu wa mafundisho, maana kuna joto hapa, nami ninajua ni kubaya. Lakini sasa, kwa mfano kama . . .Hebu nione tu kile tulichofu-. . .

12 Vema, hebu tuchukue kwa mfano, uvimbe. Sasa *uvimbe* ni nini? *Kansa* ni nini? Ni kuzidishwa kwa seli, kunatokana na seli ndogo iliyorudi nyuma. Sasa, wewe uliumbwa kutoka kwa seli moja ndogo pia. Sasa, kupitia ndoa takatifu, mama na baba yako walihusika katika kuja kwako duniani. Kwanza, ni mbegu kuto- . . ., au, kwa kweli, yai hutoka kwa mwanamke, na che—chembe hai hutoka kwa mwanamume. Sasa, kuku anaweza kutaga yai, ama ndege anaweza kutaga yai, na hata asiwe pamoja na ndege

dume, lakini halitaanguliwa kamwe, halijarutubishwa, mnaona, hana budi kuwa pamoja na mwenziwe lipate kurutubika. Sasa, na kwa hiyo...

13 Hiyo ndiyo sababu kwamba katika kisa cha Kristo wao ni...watu wengine walisema alikuwa ni Myahudi, tungetaka kuamini Yeye alikuwa Mhindi, wengine wanataka kuamini ya kwamba alikuwa Mwanglo-Sakson, wengine wanasema alikuwa Mmataifa; Yeye hakuwa yeyote wa hao, alikuwa Mungu, hakuwa Myahudi wala Mmataifa. Mnaona? Seli ya damu hutokana na jinsia ya kiume. Na katika kisa hiki, Roho Mtakatifu alimtia uvuli bikira, na akaumba Seli hiyo ya Damu, ambapo, Mungu si Myahudi wala Mmataifa, Naye alikuwa ni Damu ya Mungu, Baba Yake. Mnaona?

14 Kwa hiyo, sisi sote tumezaliwa kwa tamaa ya kujuana kimwili, na damu ndani yetu, ni damu ya dhambi, kutokana na kupotoshwa kwa njia ya kuwaleta watoto duniani. Mungu alinena tu, Adamu akatokea. Na...Kwa hiyo, mwanamke hakuwa katika uumbaji wa asili, yeye ni zaotuka la mwanamume, Yeye alitoa ubavuni mwake, u—ubavu. Naye... Adamu katika roho alikuwa mwanamume na mwanamke pia, wote wawili wa kike na wa kiume katika roho, ndipo Mungu akatenganisha ya—ya kiume na ya kike, kisha akaiweka ya kike ndani ya mwanamke, na ya kiume ndani ya mwanamume. Basi mnaona, mwili na roho, wao ni kitu kimoja. Hiyo ndiyo sababu Sara alipomcheka yule Malaika, akasema hangeweza kuwa hivyo, Mungu angalimwua mwanamke huyo papo hapo, lakini asingeweza kumdhuru, kwa sababu yeye ni sehemu ya Ibrahimu; angemdhuru Ibrahimu kama angemchukua Sara. Hiyo ndiyo sababu dhambi zetu leo, tungehukumiwa kila mmoja wetu, lakini Mungu hawezi kutuchukua kwa sababu, akifanya hivyo, anamdhuru Kristo, sisi ni sehemu Yake, sisi ni Bibi-arusi, hivi huoni? Kwa hiyo haya basi. Kwa hiyo, neema hutushikilia katika makosa yetu hadi tuweze kuona vizuri zaidi. Tunashukuru sana kwa jambo hilo.

15 Sasa, chembe hiyo ya damu, hiyo, huja...Sasa, tunajua tulikotoka. Sasa, kama ningaliweza kumchukua mtu hapa, na kumtenganisha seli kwa seli, nimrarue, ingerudi, kwa mamilioni ya seli, ingerudi ikawa seli moja ndogo katika tumbo la uzazi la mama yake, nayo seli hiyo ianze kuzidishwa. Na kila mbegu huzaa kwa jinsi yake: mbwa kwa mbwa, ndege kwa ndege, mtu kwa mtu, kadhalika. Nayo ikamzaa mtu, akaanza kukua, kukua, akijenga seli, mpaka anapofikia mahali fulani, ndipo anakoma, na yeye ni mtu mzima kabisa.

16 Sasa, tunajua mwili wako unatoka wapi, lakini ndani yako, tuseme, kuna kansa, au uvimbe, au mtoto wa jicho, ama kuvimba kibofu. Ulitoka wapi? Mnaona? Kitu hicho kilitoka wapi? Mnaona, kwanza kabisa, ibilisi hawezi kuumba, hiyo

ndiyo sababu ibilisi hawezi kuponya. Kuna Muumba mmoja tu, huyo ni Mungu.

17 Lakini, seli inayorudi nyuma, iliyochubuliwa . . . Kama vile kwenye titi la mwanamke wakati mwingine hutokea kansa ya waridi, ni kwa sababu ya mtoto mchanga, au kitu fulani kuchubuka kwenye titi lake, basi huko kuchubuka kidogo, seli hupasuka na uhai mwingine kuingia katika nyumba hiyo ya seli. Wakati seli imechubuliwa, uhai wa kansa huingia ndani yake na kuanza kuzidisha seli. Sasa, mnaona, hii hapa kansa ama uvimbe, inaendelea kuwa kubwa zaidi, zaidi, seli zikizidishwa. Inafanya nini? Kunyonya mkondo wa damu yako, ikikuua, kukutia sumu, hatimaye itakupata. Daktari, wengine wanaweza, wanaweza kufanya upasuaji, kama akiishika mapema na kuchukua, kukata kitu hicho chote kinachoizunguka, lakini kama kipande kimoja kidogo kikisalia, [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] itaendelea kukua vivyo hivyo.

18 Sasa, katika uponyaji wa kiungu hatushughuliki na uvimbe huo, tunashughulika na uhai uliomo kwenye uvimbe huo. Sasa, kwa mfano, kama ulikuwa kansa duniani, si—sishughuliki na mwili wako tu, ni—ningeshughulika na hiyo roho. Kama ninaweza kuitoa roho hiyo kwenye mwili huo, itarudi moja kwa moja mavumbini. Vema, kama unaweza kutoa uhai kwenye kansa, itachukua . . . maumbile yatajishughulikia yenyewe. Sasa angalieni, hiyo kansa inapokufa, ama huo uvimbe, vipi basi? Ma- . . . kama vile mtoto wa jicho kwenye jicho, husinyaa. Chochote kinachokufa, husinyaa, tunajua hilo. Uliza mzishi wako, mtazame akiondoa jicho la bandia, meno ya bandia, yatasinyaa.

19 Sasa, kama vile ninyi ndugu hapa, huwinda. Ukimwua kulungu usiku wa leo, ungemleta nyumbani, umweke kwenye mizani, uende ukawaambie wengine, "Kulungu huyo alikuwa na uzito wa pauni mia tatu kamili." Jihadharini asubuhi, atakuwa mwepesi kwa pauni nyingi, husinyaa. Lakini, mwache tu alale pale kwa siku chache, kisha umrudishe kwenye mizani, atakuwa mkubwa kuliko alivyokuwa mara ya kwanza. Kwa nini? Seli zinavimba, zinaoza, hiyo ni kweli, zinaanza kuoza.

20 Naam, hivyo ndivyo uvimbe ufanyavyo. Watu, kwanza wanapata ahueni, wanasema, "Whiu, jamani, najisikia vizuri. Jamani, mimi . . . Vema. Naweza kuona. Mungu asifiwe! Naweza kuona." Katika muda wa saa sabini na mbili hivi, inakuwaje? Hiyo inaanza . . . Uharibifu unaanza kuingia. Mwili wa mwanadamu, pua unabonyea. Mnaona? Unaanza kuoza. Vema, uvimbe huo hufanya vivyo hivyo ndani yako, na unapofanya hivyo, huanza kuvimba. Ndipo unasema, "Loo, nilipoteza uponyaji wangu. Nilipoteza uponyaji wangu." Huko, kutokuamini kwako kunarudisha kitu hicho moja kwa moja tena. Unaona?

21 Kama vile imani ilivyokiua, kutokuamini kunakifufua tena. "Pepo mchafu akitoka, hutembea mahali pasipo maji akitafuta mahali pa kupumzika. Kisha anarudi tena na roho wengine saba." Unaona? Sasa, kama mwenye nyumba hayupo kumpiga vita, imani hiyo, atakaporudi, "Sijali ninajisikiaje, hata iweje, najua nimepona," hiyo inamfungia nje. Sasa, unaweza kuwa mgonjwa sana, kwa sababu gani? Ni kama maambukizi mwilini mwako. Uvimbe unakufa, halafu unaoza. Nao moyo, kila wakati unapopiga, hupitia na kuisafisha damu; tunajua hilo. Damu huokota uambukizi huu, kwa sababu una homa na magonjwa, nawe unakuwa hali mbaya kuliko ulivyokuwa . . . Ndiposa watu wanafikiri wamepoteza uponyaji wao, wakati hiyo kweli ni ishara kwamba wameupata.

22 Sasa, kuna mengi tu yanayoambatana na hilo, sina wakati wa kuelezea. Mnaona? Lakini kumbukeni tu, wakati wewe . . . Sasa, sababu sichukui muda kulielezea sasa, ni kwa sababu kama unaamini kweli, hakuna kitu kitakachosimama njiani mwako, utaupata kwa vyovyote vile. Unaona? Halafu tena, juu ya Ro—Ro—Roho Mtakatifu kutangaza jambo la kufanywa, angalia, atasema ilikuwa nini, sasa ngoja kidogo, atasema kitakachokuwa. Mnaona? Usikimbie haraka sana. Ngoja. Basi kama akifanya, anajinenea Mwenyewe, *huyo* alikuwa ni mimi nikinena kwa karama, hii *nyingine* ni BWANA ASEMA HIVI, kile anachonena. Amini kwa moyo wako wote.

23 Sasa, tabia . . . Sikuzote, wewe . . . Enyi watu wote wa Kanisa la Mungu, ishini vizuri, ishini vyema, watu wanaangalia jinsi mnavyoishi. Na kama kuna jambo lolote ambalo ni kikwazo kwa Ukristo siku hizi, ni jinsi wanavyoishi wale wanaodai kuwa Wakristo: wasio waaminifu, wasioheshimika, na wanaoishi kwa njia yoyote ile. Msifanye hivyo, sisi ni Wakristo. Mtu fulani anayaangalia maisha yako, ni kweli. Kuwa mwaminifu, acha kila mtu ajue. Acha shughuli zako ziwe za haki na kweli, wa—wa—wala usichukue chochote, kisicho chako. Usiseme chochote ila kilicho kweli, nawe unaweza kusema ukweli kila wakati, naye Mungu atauheshimu ukweli. Na sikuzote fanya yaliyo mema. Mtendee kila mtu haki; wasipokutendea haki, wewe watendee mema kwa vyovyote vile. Unaona? Yesu alitutendea haki wakati hatukumtendea mema. Naye Roho Wake yuko ndani yetu!

24 Hadithi ndogo inaingia vizuri kabisa. Chini huko kusini walikuwa wakiuza watumwa, nyie watu wa Canada mlisoma habari hizo, utumwa huko kusini. Mbona, walikuwa wakizunguka-zunguka, wanawanunua kama magari ya mtumba kwa mnada, wana bili ya kuuza, wakiwauza binadamu! Sikuwahi kuamini kwamba mtu yeyote angekuwa mtumwa. Mungu alimwumba mwanadamu, naye mwanadamu akafanya watumwa. Hakuna mtu anayepaswa kuwa mtumwa chini ya mwingine, sisi ni ndugu, tunatoka katika mti mmoja mkubwa wa familia, Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni. Sasa,

kiroho tumezaliwa na Mungu, hilo hubadilisha tabia zetu.

25 Lakini ninii tu. . .Watumwa hawa walikuwa, vema, waliletwa kutoka Afrika na Makaburu, nao wakaletwa kwenye visiwa vilivyo nje ya Florida, kisha wakaingizwa, wakaingizwa kimagendo, na kuuzwa kama watumwa. Na loo, i—inasikitisha jinsi walivyotendewa. Nao walikuwa na huzuni, kamwe hawatarudi nyumbani. Wangemchukua mwanaume mkubwa mno, mwenye nguvu, labda alikuwa na mke na watoto wadogo, naye angeondolewa kwa mke huyo, na kumwuza na kumzalisha, kama ng'ombe, kwa mwanamke mkubwa, kuwaleta watumwa wakubwa zaidi ili waweze kuvuta mzigo mkubwa zaidi, na kadhalika. Loo, kama tu wanyama! Nalo halikuwa ni sawa, halikuwa sawa, hakuna wakati lilikuwa sahihi, halijawahi kuwa, na kamwe halitakuwa sawa. Na kwa hiyo basi, katika kufanya hivyo, hao watu walikuwa na huzuni, nao wangewachapa, kuwafanya wafanye kazi, kwa sababu hawakutaka kufanya kazi, walikuwa mbali na nyumbani, kamwe hawatawaona wapendwa wao tena, labda, watoto wao, baba au mama yao. Na kwa hiyo mmoja . . .

26 Wangezunguka huku na huko, madalali wangezunguka, na kununua watumwa hawa, na kuwauza tena, kama vile unavyofanya magari ama chochote kile. Wakati mmoja walikuja kwenye shamba kubwa, dalali, naye akasema, "Una watumwa wangapi hapa?"

Kasema, "Karibu mia moja na hamsini."

Kasema, "Ningetaka kuwaangalia."

27 Naye akaona jinsi ingewabidi kuwachapa wengine na kuwafanya waende, lakini kulikuwa na kijana mwanamume mmoja pale, haikuwabidi kumchapa. Ndugu, mabega yake yalikuwa nyuma, na kidevu chake juu, makini sana. Loo jamani, mtumwa tofauti jinsi gani!

Ndipo huyo dalali akasema, "Nataka kumnunua mtumwa huyo."

Lakini mwenye mali akasema, "Hauzwi."

Kwa nini, akasema, "Je, yeye ndiye bosi wa watumwa wengine?"

Kasema, "La, yeye si bosi, yeye ni mtumwa tu."

"Vema," kasema, "labda unamlisha vizuri kuliko unavyowalisha wengine."

Akasema, "La, anakula kwenye manchani pamoja na watumwa wengine."

Kasema, "Naam, ni nini kinachomfanya tofauti sana na hao wengine?"

28 Ndipo mwenye mali akasema, "Unajua, wakati mmoja nilishangazwa na hilo mwenyewe, mpaka nilipogundua, siku

moja, ya kwamba kwenye nchi ya uenyeji wake baba yake ndiye mfalme wa hilo kabila, chifu, mfalme wa hilo kabila.” Kisha kasema, “Ingawa yeye ni mgeni, mbali na nyumbani, angali anajua yeye ni mwana wa mfalme, naye anatenda kama mmoja.”

29 Ni somo la jinsi gani kwangu na kwenu! Tunaweza kuwa miongoni mwa wenye dhambi, na wageni wa duniani hapa, wasioamini, lakini sisi ni wana na binti za Mungu, wa Mfalme, Mungu. Basi na tuziendeleze tabia zetu, tuwe kama wana na binti za Mungu, tutende kama wana na binti za Mungu, na isitulazimu kusukumwa huku na huku, na kufanywa… kujaribu kusukumwa kuliamini Neno. Aminini Neno. Wana wa Mungu huamini Neno Lake, binti za Mungu huamini Neno Lake, na kwa hiyo ni lazima tufanye tabia zetu kuwa wana na binti za Mungu, Naye Roho Mtakatifu atufinyange tuwe waaminio.

30 Asanteni sana. Mungu awabariki. Nami na—natumaini kwamba Roho Mtakatifu amewafanyia jambo ambalo hamtawahi kumsahau, na mtampenda daima. Na kama sitaweza kurudi kuwaona tena, Mungu awe pamoja nanyi, nitakutana nanyi ng’ambo ya pili.

31 Nitazungumza na marafiki zangu Wahindi sasa. Huko chini kabisa kupitia mapito ya wanyama Utukufuni, nitakutana nanyi huko. Nitakuwa…nikitembea kwenye mapito ya wanyama, nitakutana na wote niwapendao, watakuwepo. Mnajua, hayo ndiyo maombi ya Wahindi mautini. Kwa hivyo, nitakutana nanyi kwenye Mapito ya Wanyama huko juu.

32 Kwenu nyinyi wazungu: Yeye anayeufanya mwezi kuangaza tupate kujua jinsi ya kuenenda gizani, na aongoze mapito yenu pia, tutakutana katika Nchi hiyo tukufu.

33 Baba yetu wa Mbinguni, sasa tunajikabidhi Kwako, tufungulie Neno. Tujalie, Baba. Tumeketi mahali hapa penye joto usiku wa leo, watu wakijipepea, hawaji hapa kuona jinsi mtu mwingine alivyovalia, wanakuja hapa kwa sababu wanakupenda Wewe. Wengi wao wamehifadhi pesa zao, wakakusanya mapeni yao pamoja na kuja mkutanoni. Jinsi tunavyokushukuru Wewe, Baba yetu. Mungu, wabariki. Loo, kama nimepata neema machoni Pako, Bwana, jibu maombi yangu kwa kila nafsi iliyoko kwenye mkutano huu. Tujalie, Mungu. Na wale ambao wamehudhuria, na wapendwa wao, wajalie haja yao, Baba, ninaomba, kama mtumishi Wako, kwa moyo wangu wote, katika Jina la Yesu. Amina.

34 Ningependa kusoma usiku wa leo, na kidogo tu…Niliwazia, nikija, nilikuwa ninaenda kuzungumza juu ya somo lingine, nami nikawazia, “Vema…” Nikiwa nimeketi pale nje kwenye gari mimi…nikisubiri, nami nikawazia…

35 Hii hapa tayari, sasa, yapata saa tatu kasoro dakika kumi na mbili. Kwa kweli, tunapaswa kuwa tumetoka katika dakika thelathini na tano, mnaona, kulingana na ratiba. Nami…Ninyi

ni wazuri sana wa kuzungumzia, siwezi kupata mahali pa kuachia, na—naendelea tu kuongea. kwa hiyo—kwa hiyo ombeni.

36 Nitazungumzia jambo lingine, kwa dakika chache tu. Kisha nafikiri nitaitisha mstari wa maombi, na kumwombea kila mtu aliye hapa ambaye anataka kuombewa, kumwombea kila mmoja. Kwa hiyo, kwamba—kwamba unahudhuria, na labda ukiamini, na unataka kuombewa, nitakuombea. Unaona? Nami nataka uamini. Sasa, tunaenda tu, kujaribu kujenga imani ndogo tu na kufanya ninii kidogo . . . zaidi sana kupiga konde mkutano, nawe usikilize kwa makini sana.

37 Na sasa nitasoma kutoka Injili ya Mathayo Mtakatifu m—mlango wa 12, kifungu cha 26 na 27, kifungu kidogo, kinachojulikana, moja kwa moja kwenye ujumbe. Sitaki kuwatwika ndugu na dada zangu Wahindi mzigo wa mambo manne au matano mbalimbali. Katika wakati huu mdogo, ni bora nibaki kwenye mstari uo huo. Wakilipata tu hilo vizuri vya kutosha, watalijua, nao wa—wanaliamini, mimi . . . kama ninaweza kujua wanachowazia. Ninaweza kusema hivyo kwa sababu najua wanaliamini, najua wanaliamini. Sasa:

> *Wanafunzi walipomwona akitembea juu ya bahari, wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakapiga yowe kwa hofu.*
>
> *Lakini* Yesu *mara moja . . . Mara Yesu akasema nao, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msiogope.*

38 Sasa, somo langu usiku wa leo ni: *Ushuhuda Baharini*, kama tulivyokuwa tukifanya leo, Ndugu Robert, kama uko hapa, *Ushuhuda Baharini,* na fungu la—langu la maneno usiku wa leo ni, "Ni Mimi; Msiogope." Kwa hiyo sasa, Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Neno.

39 Ninataka kulifanya katika mchezo mdogo wa kuigiza, kama ushuhuda. Ni wangapi wanaopenda ushuhuda? Loo, jamani! Ndugu Eddie aliniambia, kasema, "Unajua, Ndugu Branham, baada ya mikutano kwisha huko nje," kasema, "ndugu zangu Wahindi," kasema, "watakusanyika na kuanza kushuhudia, ndipo mkutano utaanza moja kwa moja kati yao, nao wataenda, wote wataenda kule." Kisha akasema, "Ndipo watatulia baada ya kitambo kidogo, kisha mtu mwingine atasimama na kushuhudia, ndipo mkutano unaanza tena." Kisha kasema, "Wanakaa tu pale, maadamu Roho yupo, wanakaa." Hiyo ni falsafa nzu—nzuri kwelikweli, si falsafa, lakini akili nzuri, ni kukaa na Roho.

40 Mnajua, popote Roho wa Mungu alipohamia, ile Nguzo ya Moto, popote ilipoenda, basi wana wa Israeli walienda pamoja Nayo. Ndipo ilipotoka katika kanisa Katoliki, huko nyuma mamia ya miaka iliyopita, Luther aliiona, naye akaenda pamoja Nayo; lakini basi akaunda dhehebu chini Yake, Mungu akaondoka moja kwa moja kutoka chini ya hilo dhehebu. Kisha

Wesley akaiona, huko Uingereza, naye akajenga kanisa lililoitwa kanisa la Wesley. Baada ya kifo Chake, yeye, na—na Whitefield, na—na Asbury, na hao, wakaunda madhehebu, naye Mungu akaondoka moja kwa moja kutoka humo. Ndipo kundi la watu walioitwa Wapentekoste, wakaiona, nao hao wakaondoka, lakini walichofanya, walifanya jambo lile lile, wakaunda madhehebu moja kwa moja kutoka chini Yake. Naye Mungu hutoka tu moja kwa moja chini ya dhehebu, anazidi kusonga. Fuata ule Moto. Sasa, na—naomba kwamba baraka tele za Mungu, juu yake.

41 Hapana shaka ilikuwa karibu wakati huu wa jioni, jua lilikuwa likitua. Ilikuwa ni siku nzuri sana, na yule mvuvi mkubwa, hayo mabega makubwa sana, yalikuwa yakiisukuma mashua hiyo kutoka ukingoni, basi alipoiondoa ile setri, mbona alipanda, na kuketi kando ya ndugu yake, Andrea.

42 Sasa, katika siku hizo hawakuwa na mashua kama tuliyokuwa ndani yake leo, iliyo na injini ndani yake inayoiendesha. Walikuwa na makasia, nao waliiita meli, wakati mwingine wametunga tanga, na kama pepo zilikuwa zikivuma, wangeweza kusafiri kwa matanga, na mbisho, kama ninyi wavuvi mjuavyo. Lakini basi, daima ni fumbo kwangu jinsi ambavyo wewe, kwa tanga hilo, unaweza kudhibiti upepo, kuukabili upepo moja kwa moja, nao upepo ukikusukuma mbele moja kwa moja kukabiliana nao; ni jinsi tu unavyoweka matanga yako. Ndivyo ilivyo kuhusu imani pia, kama unajua tu jinsi ya kuvuta matanga yako ya imani, itakufanyia jambo, moja kwa moja machoni pa magumu, inakuvusha humo moja kwa moja, ikiwa tu unajua. . .Sasa, ninyi mabaharia hapa nje mnajua ninachozungumzia. Angalieni.

43 Kisha akashika kasia lake, walikuwa na makasia marefu makubwa, wakapiga makasia mashua yao, nao wangeketi chini na kupiga makasia mara chache, kisha wanawapungia mkono kwenye ukingo watu waliokuwa ukingoni, walikuwa ndio kwanza wawe na mkutano mzuri sana alasiri hiyo. Loo, kulikuwa na mkutano wa ajabu. Mambo makuu yalikuwa yamefanywa, nao watu walikuwa na furaha sana, hata walikuwa wamesimama ukingoni wakipiga mayowe, "Kwaheri. Rudini mkatuone tena."

44 Hivi wewe. . .Unapokuwa na mkutano mzuri kama huo, ndugu, hivi huchukii kuuacha? Kama vile tu ninavyochukia kuwazia huu kuwa usiku wetu wa mwisho hapa kwa muda, nachukia sana kuondoka. Laiti tungelikuwa na takriban majuma mawili au matatu ya kukaa hapa. Na—nao walipokuwa wakiondoka, walijisikia vivyo hivyo kuhusu ndugu hao, nao walikuwa wakiwapungia mkono, "Kwaherini. Mrudisheni. Rudini mkakae pamoja nasi tena, tunataka kuwaona hapa."

45 Nao walikuwa wakivuka bahari. Loo, ilikuwa kimya sana, na laini, nayo makasia yakitumbukia majini, ambayo ni muziki

kwa masikio ya baharia, kusikia makasia hayo yakitumbukia majini. Nao wangepunga mkono wa kwaheri, na kuvuta mara kadhaa zaidi kisha wanapunga mkono kwaheri, na jinsi maskini mashua hiyo ilivyoendelea, nalo jua likishuka zaidi kila wakati. Baada ya kitambo kidogo watu waliokuwa ukingoni mwa bahari walizidi kuwa wadogo na wadogo, nayo maskini ile mashua ikawa ndogo zaidi kwao, baada ya kitambo kidogo wasingeweza kuwaona wakipunga mkono tena, wala wasingeweza kuwasikia wakiwaaga "kwaheri" tena.

46 Nao wakasema, "Lazima tuongeze mwendo." Na kwa hiyo, wakavuta kwa nguvu sana mpaka jua likatua, chini kabisa, ndipo ikawa baridi kwenye ziwa la Galilaya. Na hapana shaka ilikuwa ni yule kijana Yohana, alikuwa ni jamaa mdogo, hapana shaka alichoka haraka, kwa sababu hakuwa baharia mzee anayeparuza, kama hao jamaa wengine walivyokuwa waliozijua mashua hizo, na jinsi ya kuvua samaki, na kila kitu. Wote walikuwa wavuvi, kwa hiyo walijua jinsi ya kuvuta makasia hayo, Simoni, na Andrea, na hao wote, lakini Yohana alikuwa kijana.

47 Namsikia akisema, "Whiu, jamani! Ndugu, hmm, tupumzike kidogo, ninachoka." Basi wakayaachilia makasia, naye kijana Yohana akasimama pale huku ameinamisha kichwa chake kwa muda kidogo, nazo nywele zake nyeusi zikining'inia chini ya macho yake, naye akazichanua kinyumenyume, akasema, "Ningependa tufanye mkutano wa ushuhuda, hilo ni jambo zuri, tunapopumzika. Ningependa tufanye mkutano wa ushuhuda, nami ningependa kuwa wa kwanza kushuhudia." Mnajua, unapokuwa na jambo la kusema, kamwe huwezi kulishikilia, lazima uliseme, linafoka tu kutoka kwako, huna budi kulisema.

48 "Ningependa kuwa na mkutano wa ushuhuda," kasema kijana Yohana, "nami ningependa kuanzisha mkutano huu wa ushuhuda. Ndugu," wakati akisimama kwenye mashua, mnajua, "ndugu zangu, ningependa kusema hivi: Kwamba ni. . .Haidhuru, tangu leo na kuendelea, ni watu wangapi wanatwambia tumekosea, kamwe hawawezi kuniambia tena. Nimewasikia wakimwita Bwana wetu mpiga ramli, ibilisi, Beelzebuli, majina ya kila namna. Lakini ninajua ya kwamba wamekosea kwa kuwa, leo, ninapomwona akifanya yale aliyofanya leo, ililitatua milele kwangu."

49 Sasa, akasema, "Mnajua, wakati watu wetu walipokuja hapa kwa mara ya kwanza kutoka Misri, wakaja kupitia Palestina, nao wakaingia katika nchi hii. . .Nilikuwa nikiishi kwenye kilima juu kidogo ya Yeriko. Na kama mvulana mdogo, mvulana mdogo Myahudi, nilikuwa nikikimbia kwenye vilima na kucheza. Halafu alasiri baada ya mama yangu kunipa chakula changu cha mchana, mbona, angeniita ndani na kuniketisha chini barazani. Na katika majira ya kuchipua, ningechuma konzi kidogo ya maua na kumpa. Naye maskini

mama yangu mrembo wa Kiyahudi alizoea kuketi pale, na kukipapasa kichwa changu, na kurudisha nywele zangu nyuma, na kunisimulia hadithi za Biblia mpaka nikalala. Loo, nakumbuka hadithi hizo za Biblia!" Ni vibaya sana leo kwamba tunawaambia watoto wetu mengi kuhusu Davy Crockett, au kitu kama hicho, badala ya habari za Kristo. Tunasimulia kila aina ya hadithi zingine isipokuwa hadithi za Biblia.

50 Na kwa hiyo, basi jambo la kwanza mwajua, alisema, "Mama yangu alinisimulia hadithi kila siku. Angeniambia, 'Yohana, moja kwa moja chini ya mto hapa, sehemu ndogo, katika mwezi wa Aprili, Yoshua, yule shujaa mwenye nguvu, alizungumza na Mungu, naye Mungu akaufanyiza huo mto ukuta, nao Israeli wakavuka mto Yordani ulipokuwa umefurika, kwenye nchi kavu. Naye alipovuka, alikutana na Jemadari Mkuu wa jeshi la Bwana penye lango la Yeriko. Na jinsi, ambavyo kule nyikani, jinsi Mungu alivyowatoa watu wetu! Sasa, Yohana usisahau kamwe, Mungu, kwa nabii, Musa, chini ya Nguzo kubwa ya Moto, aliwaongoza watu wetu hadi kwenye nchi hii ya ahadi. Nawe unajua, Yohana, mvulana wangu mdogo,'" kisha kasema, "Ningeutazama uso wa mama yangu, naye akasema, 'Yohana, unajua, Mungu aliwaambia watu wetu, "Haiwabidi kuleta chochote cha kula, nitawalisha mtakapokuwa nyikani." Naye akashusha mikate, kila usiku, na akaiweka yote ardhini vizuri. Ndipo kesho yake asubuhi, yote watu wetu waliyopaswa kufanya ni kutoka nje na kuokota mikate hiyo na kuila.'"

Kisha angesema, "Unajua kwa nini . . . Nilimwambia mama yangu? 'Mama, Mungu alifanya nini? Ni nani huyo, aliyeishusha mikate hiyo?'"

"'Mungu, aliishusha hiyo mikate, na kuiweka watu wetu wapate kula, naye akawaletea kila usiku.'"

51 "Nami ninakumbuka, ndugu," angewaambia hao wengine, "nakumbuka nilikuwa nikimwambia mama yangu, 'Mama, je, Mungu ana safu kubwa mno ya tanuru huko juu na Malaika wengi wanaofanya kazi usiku? Naye huiweka mikate yote katika tanuru, na kuioka, na kisha anashuka mbio na kuitandaza chini?'

52 "Akasema, 'Hapana, Yohana. Wewe ni mvulana mdogo tu, huelewi. Unaona, Mungu ni Muumba, na si lazima Mungu awe na tanuru, Yeye hunena tu, Naye akaumba hiyo mikate.'"

53 Kisha akasema, "Ndugu, leo, nilipomwona akiwachukua wale samaki wawili wadogo na biskuti tano, mkate mdogo, na kuumega mkate huo na kuwalisha watu elfu tano, nilijua Huyo alikuwa ni Yehova yeye yule aliyewalisha watu wetu. Naye Huyu hapa angali anawalisha hata leo. Hakuna swali niani mwangu, ila kwamba . . . Angalieni jinsi alivyoonekana usoni Mwake, hakusisimkwa hata kidogo, alijua la kufanya hasa. Mnakumbuka, alitwambia kwamba alifanya yale ambayo Baba alimwonyesha. Na hapo alisimama, wakati mamia na . . .

wanaume elfu tano na wanawake na watoto, wenye njaa, wamekaa siku nzima bila chakula, kupitia kwenye mavumbi, ili tu kusikia Neno moja au mawili kutoka kwenye kinywa Chake cha thamani, amechoka, aliketi juu ya mwamba, naye mvulana mdogo aliyetoroka shuleni," mnajua, mtoro "akaenda kuvua samaki. Ndipo akamsikia Yesu, naye akapitia hapo, yeye ndiye aliyekuwa na chakula cha mchana."

54 Sasa, sikilizeni, enyi wavulana wadogo, Wahindi wadogo, na wazungu, chochote mlicho, mnaona, mvulana huyo mdogo alikuwa na biskuti tano tu na vipande viwili vya samaki. Hakikuwa kingi sana kwake, mradi tu kilikuwa mkononi mwake, lakini alipompa Yesu kile kidogo alichokuwa nacho, kiliwalisha watu elfu tano. Mnaona, hatuna mengi sana, lakini kile kidogo tulicho nacho, ikiwa tu tutampa Yeye, Yeye atakizidisha, mnaona, na kukifanya kifanye mambo makuu. Imani ndogo uliyo nayo, iweke juu Yake na kusema, "Hii ndiyo yote niliyo nayo, Bwana, lakini nitaamini na hiyo." Angalia atakayofanya nayo. Angalia tu kile kitakachotukia, dumu moja kwa moja nayo. Mtazame akikuleta kupitia kwa kila kona, na kukuleta moja kwa moja kwenye ahadi ambapo aliifanyia. Naam, Yeye anajua njia.

55 Sasa, "Ndipo nilipomwona akiwalisha hao elfu tano, amesimama pale mtulivu tu, akaumega ule mkate, nami nikapanda hapo karibu, na kupanda juu ya mwamba, nikatazama begani Mwake kuona jinsi alivyokuwa akilifanya. Akaushika mkate huo, akaumega, akamkabidhi mtu fulani, ndipo alipourudisha mkono, huo hapo tena."

56 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani, ndugu, wanasayansi, au yeyote ambaye hu-. . .Ni atomi ya aina gani aliyoachilia? Kila wakati, sio tu ngano na maziwa, ambayo huingia kwenye mkate, lakini ulikuwa tayari umekua, umeokwa, na tayari kupakuliwa. Kila wakati alipounyosha mkono Wake kuutwaa, huo hapo. Akaumega mkate huo, akawakabidhi, akaunyoosha mkono tena, ulikuwa mkate mpya tena. Aliendelea kuumega, akiwakabidhi namna hiyo, na kila wakati alipowachukua samaki hawa, samaki wadogo, samaki wadogo wa mtoni, tungewaita, heringi wadogo labda, yapata urefu huo, Naye akawapika. Kwa hiyo Yeye aliivunja tu sehemu yake, akawakabidhi, kisha akaunyoosha tena, na kulikuwako na heringi mwingine amekaangwa tayari. Amina. Loo, jamani! Sasa, hiyo ni kweli, Biblia ilisema hivyo. Hiyo hapo. Alimkuza heringi huyo, akamnenepesha, kisha akamchemsha, na kumkaanga, na kumtayarisha. Mara tu alipounyoosha mkono Wake tena, akamvunja tena, kisha akaunyoosha mkono tena, naye maskini huyo heringi akaendelea kukua, akimvunja tu namna hiyo. Na kila alipoichukua biskuti, angesema tu, "Hapa," nayo hiyo biskuti ikakua tena. "Haya basi, haya basi."

57 "Nami nikasimama pale," kasema kijana Yohana, "nao

moyo wangu ukaruka ndani yangu, kwa sababu najua katika mwili huo mdogo alikuwamo Yehova. Mungu alikuwa mle ndani, kwa sababu huyo ndiye Mungu yeye yule mama yangu alizoea kuniambia habari zake, Yule aliyeweza kuumba mkate mbinguni, naye Huyu—Huyu hapa duniani akifanya jambo lile lile." Amina. Loo!

58 Ndipo akaanza kupaza sauti. Andrea akasema, "Hebu kidogo, Yohana. Unaitikisa mashua, utaturusha sote hapa nje. Usisisimkwe sana." Alikuwa akiruka-ruka tu kote, akipiga mayowe, "Utukufu kwa Mungu!" Naye akasema, "Keti chini, Yohana. Uko kwenye mashua, utatupindua."

59 Naye Simoni, ameketi pale akitokwa na jasho chini ya ukosi, "Harakisha, Yohana, sina budi kusema jambo." Loo, jamani! Mwajua, hivyo ndivyo tufanyavyo katika mkutano wa ushuhuda. "Loo, laiti asingesema mengi sana. Laiti angetulia. Laiti ningesema kitu. . . " Hiyo ndiyo ninii. . . Loo, inabubujika tu, mwajua. Biblia ilisema zitakuwa chemchemi za maji, zikibubujika. Amina. Kamwe usingeweza kuzituliza.

60 Yesu alimwambia yule mwanamke kisimani, maji ambayo Yeye anatoa yatakuwa visima vinavyobubujika. Whiu, jamani! Nami nawaambia, baada ya kuona mkutano huo siku hiyo, wote walikuwa wakibubujika kule kwenye bahari hiyo.

61 Basi maskini Yohana hatimaye alilazimika kuketi chini, maana Simoni mkubwa aliinuka. Akasema, "Mwajua, Andrea, ndugu yangu hapa, sasa, kaa kimya, wakati Andrea alipokuja kuniambia kuhusu, alikuwa amemwona Masihi, nisingeweza kuamini upuuzi kama huo, kwa sababu nilikuwa msomaji wa Biblia, ninajua kile Biblia ilisema. Kwa hiyo, siku moja yeye. . . baada ya kuosha nyavu zetu na kuingia, nilipelekwa Mbele za Yesu. Nami nakumbuka, siku moja, wakati baba yangu mzee. . . Ninyi nyote mnamjua, loo, yule Farisayo, mwaminio shupavu kwelikweli. Tulikuwa tumeishiwa na chakula, hatukuwa na chakula chochote. Nasi tulikuwa wavuvi, tuliishi kando ya bahari. Naye baba yetu alikuwa ametufundisha kuvua samaki, baharini, tupate riziki, alikuwa akitulea sisi wavulana kuwa waaminifu, na kufanya yaliyo mema. Nami ninaweza kumwona baba yangu mzee na hizo nywele zenye mvi zikining'inia chini.

62 "Basi tulipoenda siku hiyo. . . Naye mama tayari alikuwa ameenda Utukufuni, na ni Andrea tu, na mimi, na baba. Nasi tulikuwa na madeni fulani, basi asubuhi hiyo kabla hatujaondoka, loo, ninaweza tu kumwona baba yangu mzee akipiga magoti kando ya mashua hiyo, na kusema, 'Yehova Mkuu, Wewe ulisema, "Usiwe na deni yoyote ya mtu," nami nina deni. Sijaweza kuvua samaki yeyote. Hakuna hata mmoja wa hao wengine ufuoni humu anayewavua samaki wowote, hawakimbii kamwe. Lakini, Mungu, Wewe ndiwe Muumba,

ninahitaji samaki sana, si utanisaidia leo hii kuvua samaki?' Basi siku hiyo tulivua shehena ya ajabu ya samaki.

63 "Nasi tulipoingia, na tulikuwa tumeosha nyavu zetu, nakumbuka baba akiketi na kunikumbatia kwa mkono wake, na kusema, 'Simoni, mvulana wangu mdogo, baba anazeeka, itanibidi nikaungane na watu wetu hivi karibuni. Maishani mwangu mwote, enyi wavulana. . . Njoo hapa, Andrea, uketi gotini mwangu. Maishani mwangu mwote nimeamini kwamba ningemwona Masihi. Niliamini ningemwona Kristo, ambaye watu wetu wote wamemngojea, kwa maelfu haya ya miaka, na hapana shaka, lakini sasa, sitamwona, kwa maana siku zangu zimekaribia kwisha, lakini ninyi wavulana huenda mkamwona. Sasa, sitaki nyinyi mchanganyikiwe na mshindiliwe mitindo ya kisasa ya ulimwengu, lakini nataka ninyi wavulana mkumbuke kwamba ajapo Masihi, atakapokuja, kumbukeni Maandiko yanasema atakuwa nabii kama Musa.'

"Nami namkumbuka baba yangu mzee, nakumbuka tulipomzika."

Andrea akitikisa kichwa chake, "Hiyo ni kweli."

64 "Basi wakati mimi na Andrea tulipoenda mbele za Yesu, alinitazama na kusema, 'Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.' Loo," akasema, "hiyo ilitosha milele, papo hapo! Nilijua Huyo alikuwa *yule* Nabii, kwa sababu si kwamba tu alinijua mimi, bali Yeye alimjua yule mzee baba yangu mtauwa, aliyekuwa amenifunza kuliamini Neno la Mungu daima, na kwamba Masihi atakuwa Nabii. Alimjua na yeye pia, hilo lilitosha kwangu."

65 Na bila shaka, wakati huo Filipo alikuwa akimgeukia Nathanaeli, akicheka tu, mwajua, akasema, "Je, ni sawa, Nathanaeli?"

Akasema, "Endelea, Ndugu Filipo."

"Vema, mnajua nilipoona hilo likifanywa, nilikimbia kuzunguka kilima nikamtafute Nathanaeli, kule. Na vipi kuhusu hilo, Nathanaeli?"

Akasema, "Hebu niisimulie! Hebu niisimulie!"

"Vema, usiiyumbishe mashua. Keti kimya."

66 Akainuka, akasimama na kuanza kuongea, mwajua. Akasema, "Vema, sikuzote nilikuwa. . . Mimi na Filipo tulikuwa tumejifunza Maandiko, nasi tulijua kwamba—kwamba kanisa la kisasa halikuwa na mwelekeo wake, kwa muda mrefu, kwa sababu walikuwa wakitazamia *tabaka* fulani kutoka Mbinguni. Wala hawakuamini ya kwamba—kwamba yuaja Mungu, lakini sisi tuliamini ya kwamba Mungu atakuwa Mwanadamu."

67 Linapaswa kuwa la kushangaza. Mungu alipobadilisha kinyago Chake, Mungu alipofanyika Mmoja wetu kusudi atuokoe, ilimbidi. . . Katika Agano la Kale, ilikubidi, kabla

hujaweza kukomboa, ilibidi uwe mkombozi wa jamaa. Hadithi ya Ruthu inaleta hilo vizuri. Mnaona? Ilibidi uwe wa jamaa, na ilimbidi Mungu awe wa Jamaa yetu, awe Mmoja wetu. Wazia Yehova Mungu katika hori akilia kama mtoto mchanga, mwazie akicheza kama Mvulana, mwazie akijenga nyumba kutokana na mbao zenyewe alizoziumba Yeye. Amina.

68 Waliamini angekuwa, Naye angekuwa yule Nabii mkuu. Nathanaeli akasema, "Nilipoenda mbele ya uso wa Bwana Yesu, kidogo nikishuku yale Filipo aliniambia, na Filipo akaniambia, kasema, 'Mbona, hata anaweza kukwambia wewe ni nani ukifika huko, isingenishangaza.'" Lakini akasema, "Nilipoenda mbele ya uso Wake, alisema, 'Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake!' Nami nikamwambia, 'Rabi, ulinijua lini Wewe?' Kasema, 'Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.' Hilo lilitosha.

69 "Nanyi mnajua nilichofanya, ndugu? Mlikuwepo. Nilikimbia moja kwa moja, na kuanguka miguuni Pake, na kusema, 'Rabi, Wewe ndiwe Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.' Na hapo alisimama mchungaji wangu pale pamoja . . . akalipuka kama chura, ameketi pale akinitazama, lakini haikuleta tofauti yoyote wakati huo, kwa sababu nilikuwa nimeona kitu halisi. Nilikimbia pale hata hivyo na kuliamini," kasema, "kwa sababu nilijua Biblia ilisema hivyo ndivyo hasa angefanya."

70 Loo, hivi hatuwezi kuanzisha mkutano wa ushuhuda usiku wa leo? Yale ambayo Mungu alisema angefanya katika siku za mwisho, tunayaona yakitendeka. Amina. Haileti tofauti yoyote kile mtu mwingine yeyote anasema. Kama wanataka kuwa Presbiteri, Anglikana, ama chochote wanachotaka kuwa, hiyo ni sawa, hiyo ni juu yao. Lakini tumeona jambo fulani, tuliona Maandiko katika siku za mwisho yale ambayo angefanya, nasi tunamwangalia akimwaga Roho Wake juu ya mahali pale. Haleluya! Na kuona ishara na maajabu yakitimizwa, kuona Uwepo hasa wa Kristo aliye hai ukimdhihirisha Mwenyewe. Na sasa, kote katika Maandiko, ambapo Yeye alionyesha ishara Yake ya mwisho kwa kizazi, ambacho kiliimaliza. Na hapa tunaona ishara ya mwisho ya kizazi hiki, kama Yeye alivyosema, katika wakati wa jioni, ingetukia.

71 Sasa. Loo, hapana shaka walikuwa na ushuhuda hali-. . . Andrea akasema, "Ndugu, naweza kusema neno moja tu? Ningependa kusema jambo. Je, mnakumbuka wakati tulipopanda kwenda Sikari, nasi tukatumwa, kwenda mjini, kununua chakula? Ndipo tuliporudi . . . Bwana wetu asingeingia mjini pamoja nasi, bali aliketi na kupumzika. Basi tuliporudi, tulisikia mtu akiongea, nasi tukanyemelea nyuma ya kichaka, tukatazama juu ya kile kichaka, na pale alikuwako mwanamke mwenye sifa mbaya, mwanamke mbaya, kahaba, akiongea na Bwana wetu. Mnakumbuka jinsi tulivyoshangaa? Tuliwazia, 'Mwanamke kama huyo, akizungumza na Bwana wetu?

Mwangalieni akimfokea, mwangalieni Yeye akimfukuza Mbele Yake.'" Hivyo ndivyo wangali wanafikiria. Yeye hafanyi hivyo.

72 "Lakini tukagundua ya kwamba Yeye alimwomba fadhili. Akasema, 'Nipe maji ninywe.' Vema, tunajua kwamba hakuna rabi, au hakuna hata mmoja wa Mafarisayo wetu ambaye angeweza kamwe kumwomba mwanamke kama huyo amfanyie lolote. Lakini huyu hapa Bwana wetu, Mungu wa uumbaji, ameketi hapa katika mwili wa nyama na kumwomba mwanamke mwenye sifa mbaya ampe maji anywe, amhudumie." Amina.

73 Hilo ndilo linalomfanya Mungu kwangu mimi, kwa sababu alijinyenyekeza. Mungu ni unyenyekevu, kamwe usisahau hilo. Unyenyekevu ni Mungu. Pasipo majivuno, sikuzote ni unyenyekevu.

74 "Nasi tukamsikiliza. Tuliwazia, 'Hakika katika dakika moja atanyakua fimbo na kumfukuza ashuke, mjini anamoishi.' Lakini akasema, 'Nipe maji ninywe,' nao. . . wakaanza kuzungumza juu ya dini. Akasema, 'Tunaabudu katika mlima huu; mnasema huko Yerusalemu,' na kadhalika, Naye akazungumza naye kwa muda kidogo. Na baada ya kitambo kidogo, akamwambia, 'Nenda, kamwite mume wako mje naye hapa.' Naye akageuka na kusema, 'Sina mume.' Mnakumbuka?"

75 Mathayo akasema, "Naam, nakumbuka." Yeye ndiye aliyeiandika, mnajua. Akasema, "Loo, naam, na—nakumbuka, moyo wangu ulizimia. Nikawazia, 'Jamani, jamani! Uh-huh! Huyo hapo Bwana wetu amekosea wakati mmoja.' Mnaona? Kwa sababu alimwambia alikuwa na mume, nenda kamwite mume wako, naye akasema, 'Sina mume.' Kisha akageuka na kusema, 'Umesema kweli.' Ndipo sote tukashangaa. Hapa anasema, 'Nenda kamwite mume wako,' akasema, 'Sina mume,' Yeye akasema, 'Hiyo ni kweli.'

Tazama. "Nenda kamwite mume wako."

"Sina mume."

"Umesema kweli."

76 Sasa, "Loo, sote tulishangaa, na mioyo yetu ikadunda, nasi tukainuka juu ya vichaka nyuma Yake ili kuona kile ambacho angesema tena. Loo, alikosea! Akasema, 'Sina mume,' na hata hivyo tulimwamini kuwa ndiye Masihi. Hiyo ishara kuu ya Kimasihi ingekoseaje? Nasi tulijua Yeye alikuwa ni Masihi, kwa sababu alifanya ishara ya Masihi. Kwa hiyo sisi. . ." Masihi ni Mungu, aliyetiwa mafuta, na aliyetiwa mafuta ni Neno, nalo Neno lilidhihirishwa. Mnaona? "Tunajua ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Naye Huyu hapa, kila wakati ilikuwa sahihi ila wakati huu, lakini sasa ilikuwa imekosea, kwa maana alimwambia yule msichana, 'Nenda kamwite mume wako,' akasema, 'Sina.' Akasema, 'Umesema kweli. Umesema kweli, kwa kuwa umekuwa na watano, na huyo unayeishi naye sasa siye wako.'" Loo!

77 “Nasi tukaona vile mwanamke huyo alisema. Aligeuka kwa macho ya mshangao, naye akasema, ‘Bwana, naona ya kuwa Wewe u Nabii.’” Sasa, hilo, kwa kweli, katika King James limetafsiriwa vibaya. Ni sawa, ni sawa hivyo. Lakini kama utachukua maandiko yako ya pambizoni juu ya hilo, na kulifuatilia katika Kiyunani asili, na wengi wa wanachuoni hapa hulisoma, ilisema, “Wewe ndiye *yule* Nabii.” Mnaona? Hayo ndiyo maandiko ya pambizoni, “Wewe ndiye *yule* Nabii.” “‘Naona ya kuwa Wewe ndiwe *yule* Nabii. Sasa tunajua kwamba ajapo Masihi, aitwaye Kristo,’” *yule* Nabii, Masihi, na Kristo, wote Mtu yule yule, “‘ajapo atatuambia mambo haya yote.’

“Naye Yesu akasema, ‘Mimi ninayesema nawe, Ndiye.’

78 “Ndipo mwanamke huyo akakimbilia mjini na kuanza kuwaambia wanaume wote, ‘Njoni mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya,’” sasa, angalieni, “‘aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyo kuwa ndiye Masihi mwenyewe?’ Nanyi mwajua, sote tuliingia mjini tupate kujua yaliyotukia, ndipo wanaume wote katika mji ule wakaamini ushuhuda wa yule mwanamke. Loo, ilikuwa wakati mzuri sana!”

79 Yapata wakati huo Mathayo akasema, “Ngoja . . . ” au akasema, “Ngoja kidogo. Nataka . . . Nina jambo nataka kusema. Hebu nishuhudie upesi sana.” Kidogo wakati ulikuwa unachelewa, mwajua. “Hebu nishuhudie.” Kasema, “Mnakumbuka wakati ule ambapo dada yetu, Rebeka . . . Aliishi Yeriko. Naye Bwana wetu akashuka kwenda—kwenda kula chakula cha kutwa huko Yeriko, nasi tukaingia mjini. Nanyi mnakumbuka Rebeka akishuhudia? Loo, mnakumbuka, alikuwa amesihi katika kila mkutano, ‘Ombeni kwamba mume wangu aokoke. Ombeni, mume wangu ataokoka.’ Jina lake lilikuwa Zakayo, yule jamaa mdogo.” Alikuwa mfanyabiashara. Hebu tuamini kwamba alikuwa na mkahawa, naye alikuwa na utungo mkali, ushindani, hasa, naye alikasirika sana kwa sababu Yesu alikuwa anaenda kula mahali pengine, kana kwamba mahali pake hapakuwa pazuri vya kutosha.

80 “Naye Rebeka sikuzote aliomba. Akasema, ‘Zakayo, u—unaweza kuwa na washindani wengi, na unaweza kuwa unapendwa na Rabi Levinski, kuhani, yule rabi ambaye huja na kula pamoja nawe,’” kwenye Klabu ya Kiwanis, au chochote kile. “‘Unaweza kuwa unapendwa naye, lakini hebu nikwambie kitu, Mtu huyu ni Nabii. Naye . . . ’

81 “‘Mbona, unajua rabi wetu aliniambia nini? Kwamba hatujakuwa na nabii tangu miaka mia nne iliyopita, kwa kuwa Malaki alikuwa ndiye nabii wetu wa mwisho. Nawe uniambie kwamba Jamaa huyo, aliyezaliwa kule chini kando ya bahari, kimoja cha hivyo vibanda vidogo, mahali fulani kule chini, angekuwa Nabii? Ai, Rebe- . . . ’” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

82 “Tulijua kama angewahi kuketi chini na kuzungumza na Yesu, angeshawishika.” Na hilo ni jambo lile lile siku hizi. Kama utaketi tu chini, uzungumze Naye kwa dakika chache, utajua. “Kwa hiyo, mnakumbuka yale Rebeka aliyotwambia? Sasa, nitarudia ushuhuda wa Rebeka,” akasema Mathayo.

83 “Sasa, mnajua, usiku kucha maskini mzee Zakayo hakuwa na utulivu.” Unajua, unapoanza kumwombea jamaa fulani, kwa namna fulani anaingia katika hali mbaya. Kama unataka mtu fulani aokolewe, ama jambo fulani lifanyike, anza tu kuwaombea. Hiyo ndiyo sababu hatuninii. . .Maombi ndilo jambo kubwa zaidi lililowahi kuwekwa mikononi mwa mwanadamu; maombi hata humbadilisha Mungu. Mungu alitangaza kifo juu ya mtu wakati mmoja, akaelekeza uso wake ukutani na kuomba, naye Mungu akamhifadhi kwa miaka kumi na mitano zaidi. Kweli. Ni kweli.

84 “Kwa hiyo tunaona kwamba maskini huyo Rebeka aliomba kila wakati. Na usiku huo hakuweza kulala. Alichungulia kwa kona ya jicho lake, akasema. . .Zakayo alihangaika. Akasema, ‘Bwana, najua unamshughulikia, najua unamshughulikia. Sasa, Yesu, yule Nabii, anakuja mjini kwa ajili ya mkutano huu, hapa chini, nami nataka sana amwone. Bwana, fanya njia sasa. Mfanye tu mwenye mashaka; mnyime tu usingizi.’

“Huyo hapo, asingeweza kulala. Kwa hiyo, basi, hilo ni sawa. Kwa hivyo, kesho yake asubuhi. . .Alikuwa amesinzia akalala, akilala akiomba usiku kucha.”

85 Na kama unataka mume wako aokolewe sasa, fanya jambo lile lile alilofanya Rebeka, anza tu kumwombea. Nawe unajua, huko nje kwenye bahari ile wakati yuko huko nje akivua samaki, ama kule chini katika biashara, atashawishika sana asiweze hata kulala. Naam, bwana. Hiyo ni kweli. Anapata tu. . .Na kama unataka mke wako aokolewe, fanya jambo lile lile, naye atatoka kwenye kila chama cha karata na kila kitu kingine anachoshiriki. Hawezi tu kujiepusha nalo. Hakika atalifanya. Naam, bwana. Loo, kuna nguvu nyingi tu katika maombi!

86 “Naye akasema aliomba, halafu basi karibu asubuhi akaenda kulala. Mara akaamka, kabla ya mapambazuko, Zakayo alikuwa tayari ameamka, akavaa nguo zake nzuri kuliko zote, naye akasema, ‘Asante, Bwana. Najua, najua unamshughulikia.’ Na kwa hiyo akageuka, akasema, ‘Loo, mpenzi, ni kitu gani kimekuamsha mapema hivi?’

87 “‘Loo,’ akasema, ‘hakuna kitu. Niliwazia tu ningetoka nje nipumue hewa safi kidogo.’” Unajua jinsi unavyoweza kupata kila aina, udhuru, unaona. “‘Ninaamini nitatoka tu na kupumua lundo la hewa safi. Unajua, kidogo humu chumbani si safi.’

88 “‘Naam,’ akawazia, ‘tumefunga ndoa miaka ishirini na mitano, wala kamwe hakufanya hivyo hapo kabla, kwa hivyo hapana shaka kuna shida fulani sasa. Kwa hiyo, tunajua

kwamba...Naye Yesu anapaswa kuwa hapa karibu wakati wowote, kwa hivyo nitafanya tu kana kwamba sijali. Lakini haamini kwamba Yesu ni Nabii, kwa hiyo laiti angaliweza kushawishika kwamba Yeye ni Nabii, ndipo angejua Neno la Bwana, maana yeye ni Myahudi, naye anajua Neno humjia nabii. Kwa hiyo anajua kwamba angekuwa na Neno la Bwana.'

89 "Basi akamwangalia, naye akajivalisha nadhifu kabisa, kisha akachanua ndevu zake, na kurudisha nywele zake nyuma, halafu akavaa kilemba chake kilicho kizuri mno. Naye akashuka kupitia kwenye njia ya mguu, akiangalia nyuma kuona kama Rebeka anamwangalia, naye yuko kwenye dirisha lingine, akichungulia nyuma ya dirisha namna *hii*, akiona anachofanya. Akapiga magoti na kusema, 'Asante, Bwana, asante. Anashuka moja kwa moja kwenda kuliona. Najua utayajibu maombi yangu.'" Hivyo ndivyo unavyopaswa kuamini, Mungu atakufanyia jambo hilo.

90 "Kwa hiyo basi, anatoka nje, mwajua, na kushuka barabarani, naye anaangalia pande zote. Sasa, kama atafanya hivyo, angepanda *huku* chini ya miti, lakini badala ya kufanya hivyo, alishuka moja kwa moja kuelekea lango la kusini ambako Yesu aliingilia. Mnaona?

91 "Ndipo anashuka kule chini, aliwazia, 'Nitashuka huko mapema,' akasema moyoni mwake, akitoa ushuhuda baadaye, 'Nitashuka kule mapema, nami nitamwona huyu hapa nabii wa uongo, *anayejiita* Nabii wa Galilaya. Atakapopitia hapa, nitamwambia ukweli wa mambo.'" Um-hum. Hamtambui, mnaona, wanapoudhika kwa upesi sana, kumbuka tu Mungu angali anashughulika, mnaona, Yeye anajua jinsi ya kufanya hilo.

92 "Basi mnajua nini? Alipofika kule chini, mtaa tayari ulikuwa umejaa watu, walikuwa wamekaa pale usiku kucha wakimngojea." Mnajua, Yeye alikuwa na marafiki pia. "Ndipo akashuka kule chini naye alikuwa mdogo sana, huenda alikuwa mkubwa katika kusanyiko lake mwenyewe, bali alikuwa tu ni mtu mwingine katika hilo."

93 Mnajua, naipenda dini hii ya kale, itamfanya mwenye suti rasmi kukumbatiana na mwenye ovaroli na kusema, "Ndugu!" Itafanya aliyevaa nguo ya kaniki na a—na a—aliyevaa ya hariri kukumbatiana, waseme, "Dada!" Haina upendeleo, wewe ni mtu mwingine tu. Haijalishi unamiliki nini, au wewe ni nani, wewe ni mtu mwingine tu. Hakuna mabwana wakubwa kati yetu, sisi sote ni watoto wa Mungu. Hiyo ni kweli. Uh-huh. Loo, jamani!

94 "Basi huyu hapa anashuka pale, ndipo akawazia, 'Watakaponiona, Zakayo, mfanyabiashara mkuu wa mji huu akishuka chini, wote watasimama kando, na kusema, "Mheshimiwa, bwana,"' lakini wakagundua kwamba alikuwa ni mtu mwingine tu. Naye akafika pale, alikuwa mdogo sana

miongoni mwao, yeye. . .hakuna mtu. . .asingeweza kumwona Yesu. Akasema, 'Unajua nini? Sasa, hii. . .Anaingia. . .Hii ni Barabara Kuu ya Utukufu, sasa, hana budi kuvuka Kivuko cha Haleluya kule juu, kwenye mtaa unaoitwa Barabara Kuu ya Haleluya.'"

95 Yeye sikuzote hupitia kwenye mitaa hiyo, Utukufu, na Haleluya, na Amina, na Mungu Asifiwe. Yeye sikuzote husafiria barabara hizo, simama tu hapo, utaipata baada ya kitambo kidogo.

96 "Basi akakimbia barabarani upesi sana, haraka alivyoweza, kisha akapanda hadi Barabara Kuu ya Haleluya. Naye akasema, 'Sasa, nitasimama papa hapa, papa hapa pembeni.' Ndipo ikatokea aliwazia, mwajua, 'Kuna msongamano mkubwa sana, nao unazidi kuongezeka wakati wote, na wakati Yeye atakapofika hapa, watapita tu juu yangu. Kwa hivyo mnajua ninachoamini nitafanya? Nitaamini nitapanda juu ya mkuyu huu hapa, ndipo basi nipate kumwona vizuri.'

97 "Kwa hivyo akaruka, yeye ni mfupi sana, asingeweza kulifikia tawi. Kwa hiyo, akaangalia pale, naye mkusanya taka wa jiji alikuwa bado hajakusanya takataka. Kwa hiyo akanyoosha mkono, na kushika ndoo ya takataka, naye huyu hapa anakuja." Loo, unajua, kama umeyakinia kumwona Yesu, atakufanya ufanye mambo ambayo hukuwazia ungefanya. "Loo, jamani! Huyu hapa, mfanyabiashara wa mjini, amebeba pipa la takataka. . .ndoo.

98 "Ndipo yapata wakati alipofika hapo, mshindani wake akamwona." Sijui kama mtu fulani anayeketi hapa usiku wa leo amefichuliwa namna hiyo, ninii tu, loo, kuanikwa. Sijui kama ungeweza kuwa, unayeketi hapo. "Loo, jamani! Sikutaka mtu yeyote anione humu ndani." Lakini mnajua, Yeye anajua ulipo hasa.

99 "Na kwa hivyo basi akaliweka maskini hilo pipa chini, naye mshindani akasema, 'Loo, naona amebadili wadhifa wake, kutoka kwa mfanyabiashara, sasa, yeye ni mkusanya taka za mji.'

100 "Na kwa hiyo hakujali, maskini uso wake mwekundu, lakini aliyakinia kumwona Yesu. Mnaona? Alitaka kumtazama Yeye, hakuamini Yeye alikuwa nabii. Na kama hakuwa nabii, alikuwa anashuka moja kwa moja kule na kumwambia kuhusu jambo hilo, hivyo tu. Alitaka kusema, 'Vema, wewe ni mdanganyifu, hupaswi kuwa katika mji huu.'"

101 "Kwa hivyo akapanda juu ya pipa la takataka na kuparamia juu ya m-. . . " Uh-oh. Hamlitumii neno hilo hapa *kuparamia* sivyo? Hapana. Hilo ni la kusini. . .Hilo linamaanisha "kupanda juu ya mti," mwajua, kujishikilia kwa magoti yako. Tunakuita *kuparamia* (huko chini) juu ya mti. "Akapanda juu ya huo mti, akafika kule juu, ndipo akaona ambapo matawi mawili

yanakingamana namna *hii*, naye akaketi juu ya yote mawili." Hapo ndipo sote tunapofikia, ambapo njia mbili zinakutana: yako na ya Mungu; hapo ndipo unapofanya uamuzi wako.

102 "Akaketi pale juu, angalieni, akiwa amejinadhifisha vizuri sana, akipangusa takataka kutoka kwake, akitoa vibanzi mikononi mwake. Ni mchafuko wa jinsi gani! Lakini alitaka kumwona Yesu."

103 Itakufanya uingie katika mchafuko. Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi, hawapendi kuzaliwa upya, wanajaribu kukufanya kitu kingine. Wanataka kupeana mikono, waseme, "Ninamwamini Mungu Mwenyezi, Baba. Ninaamini Kanisa takatifu la Katoliki ya Kirumi, ushirika wa watakatifu, na—nami ninamchukua kuwa Mwokozi wangu. Nimezaliwa mara ya pili." Uh-uh. La, la. La. Sikiliza, ndugu, kuzaliwa upya ni zaidi ya hayo. Sikiliza, nataka, nikwambie jambo, kuzaliwa kwokwote ni mchafuko, sijali kama kuko kwenye zizi la nguruwe, au kama kuko kwenye chumba cha hospitali, kuzaliwa kwokwote ni mchafuko. Na hebu niwaambie, kuzaliwa upya si chochote pungufu, ni mchafuko, utalia vikali, na kupiga mayowe, na kuosha rangi yote kutoka usoni mwako kwa machozi, lakini i—itabidi ufe, bali huleta Uhai mpya. Hilo ndilo jambo kuu, kutaleta Uhai mpya, na utakuwa kiumbe tofauti. Kutakuletea mchafuko, lakini hu—huna budi kufanya hivyo upate kuzaliwa mara ya pili, huna budi kuchafuka, unaona, bali kutaleta Uhai mpya.

104 "Naye huyu hapa ameketi huko juu, akijikwangua, imwondokee. Nanyi mwajua, alisema, 'Sasa, Rebeka aliniambia . . .' Naye alikuwa nyumbani, akiruka-ruka, akisema, 'Mungu, najua unajibu maombi. Haleluya! Ataupata leo, hamna lingine, kwa sababu hakurudi. Alikuwa ametoka akatembea kwenye njia ya mguu na kurudi ndani ikiwa alitaka hewa safi kidogo, lakini alienda haraka alivyoweza, nami nilimwona akielekea Barabara Kuu ya Haleluya haraka alivyoweza kwenda. Najua, Bwana. Asante tayari, yajibu maombi.'

105 "Hivyo basi, ilikuwaje? Ndipo huyu hapa maskini Zakayo ameketi huko juu, naye akasema, 'Unajua, Rebeka alisema Yeye alikuwa ni Nabii. Sasa, mtu fulani anaweza kuniona hapa juu, na kumwonyesha nilipo, kabla sijapata nafasi nzuri ya kumwambia ninachomwazia juu Yake.' Basi akanyoosha mkono, akashika hayo matawi, akayavuta na kujifunika nayo pande zote, na kujificha, akaketi nyuma katika . . . mwajua, kama kunguru anayeketi huko nyuma m—mtini. Akarudi kule nyuma kabisa, na akajificha.

106 "Alikuwa na jani moja kubwa la mkuyu *hapa*, akalifanya hilo dirisha, angeweza kuliinua na kuchungulia, kisha analirudisha chini. Mnaona? Na moja kwa moja akasikia kelele." Mnajua, kuna jambo fulani la ajabu, karibu kila mahali Yesu anapoenda,

kuna kelele nyingi. "Alisikia . . . Akasema, 'Vema, hapana shaka anakuja, kelele nyingi.'

107 "Basi baada ya kitambo kidogo, huyu hapa anapiga kona, ndipo anapopiga kona, inaonekana, makutano wamemzunguka kote, watu wanne au watano wakiwazuia watu wasimkaribie, ndipo anapiga kona. Akasema, 'Maskini jamaa yule mdogo?'"

108 Mnajua, Biblia ilisema, "Hana uzuri, hata tumtamani." Hakuonekana kama mfalme fulani mkubwa, ama kuhani, ama chochote kile, Alikuwa mnyenyekevu, Jamaa mdogo, akitembea pale ameinamisha kichwa Chake, kichwa chini, akashuka moja kwa moja mpaka akafika papo hapo chini ya mti, naye huyu hapa maskini Zakayo ameketi pale juu, mwajua, akiinua jani hili, mwajua, akichungulia *hivi*. Na mara tu yapata wakati alipofika chini ya ule mti huku ameinamisha kichwa Chake, aliangalia kule juu, akasema, 'Zakayo, shuka; ninaenda pamoja nawe nyumbani kwa chakula cha kutwa.'" Utukufu!

109 Je, alikuwa Nabii? Amina! Hakika alikuwa. Si tu kwamba Yeye alijua alikuwa mtini, bali alijua jina lake lilikuwa Zakayo. Amina. Utukufu!

110 Hapana shaka ilikuwa Nathanaeli aliyesema, "Hebu kidogo. Mnakumbuka wakati ule ambapo maskini yule Farisayo aliendа na kumwalika kwenye chakula cha jioni pamoja naye?"

"Naam."

111 "Hawakutualika, wala tusingeweza kuja bila mwaliko, lakini Yeye akaenda, nao wakamwacha aketi mle na miguu michafu. Kumbukeni maskini mwanamke yule alichukua dinari yake ya Kirumi akashuka kule, na kununua kibweta cha marhamu, kisha akajipenyeza mle ndani, naye alikuwa amesimama pale karibu na miguu Yake, na—na hapo ameketi Yesu na miguu michafu." Loo, linasikika la kukufuru kusema jambo hilo, lakini walifanya hivyo.

112 Unajua, unapoingia kwenye nyumba zao kule, jambo la kwanza wanalofanya, wa—wanamchukua mtumishi mwosha miguu, sasa, huyo ndiye mtu mwenye mshahara mdogo kuliko wote katika kundi hilo, ni mtumishi mwosha miguu, anaenda huko nje, ndipo mgeni anapoingia, anaishughulikia miguu yake. Naye anamtoa makubadhi yake na kuosha miguu yake, kwa sababu walikuwa . . . walitembea barabarani, nao wanyama walipitia barabara hii, mnaelewa, ambapo wanyama walikuwa, na—na walikuwa wameingia kwenye vumbi. Na—nao walipotembea, walikuwa wamevaa joho, nalo likaokota mavumbi hayo, nayo yakatua kwenye viungo vyao na kadhalika. Na, loo, huo uvundo kutoka kwa hao wanyama! Na kwa hiyo ha—haikuwa—haikuwa vema kuingia nyumbani.

113 Kwa hiyo walikuwa na mtumishi mwosha miguu, alikuwa ndiye mtu anayelipwa mshahara mdogo kuliko wote, naye angeenda huko, na kuwaosha miguu, na kisha—na kisha

kuwakaribisha, mnaona, wanawavalisha jozi safi ya makubadhi. Ndipo Yesu akawa Mtumishi mwosha miguu, kazi duni kuliko zote duniani, na huku mtu fulani akashindwa kuosha miguu Yake.

114 Halafu basi, jambo lingine wanalofanya, jua la Palestina, miale hiyo ya moja kwa moja ilikuwa joto sana, kwa hiyo ingeunguza shingo zao na uso wao, nao wangewapa marhamu, na kuwatoneshea pale, na kunawa uso wao nayo namna *hiyo*, nayo ikawabaridisha, ilibaridisha, kama mentha. Nayo ni baridi, hutokana na tumba la waridi walilolipata juu sana milimani. Malkia wa Sheba alileta lundo lake Israeli alipokuja katika siku za Sulemani. Kisha wangeipangusa.

115 Halafu wao. . .Halafu jambo lingine, wangekaribisha m—mgeni wao kwa busu. (Njoo hapa, ndugu.) Hivi ndivyo walivyofanya, wangeshika mikono yao namna *hii*, nao walipoingia, walikaribishwa. Wangekumbatiana namna *hii*, kisha wakabadilishana mikono namna *hii*, papa hapa, na upande *huu*, nao wangali wanafanya hivyo, kuwabusu shingoni, kuwapa makaribisho. Mnaona? Busu la makaribisho.

116 "Vema, huyu hapa ameketi Yesu. Huyu hapa mzee, maskini rabi mkubwa, amesimama pale, mwajua, na divai yake yote, na—na vyakula vyake vyote vizuri huko nje. Nao hao maskini, wasingeweza kuja, na, kunusa, wangenusa harufu hiyo nzuri, mwana-kondoo aliyeokwa, mwajua, na loo, jamani, jinsi walivyotamani kuja, lakini wasingeweza kuja. Inatia hamu sana!" Loo, hao marabi, walipata pesa, nao wangeweza kufanya karamu kubwa. "Kwa hiyo, naye Yesu alikuwa ameingia, na hao wengine wote walikaribishwa, Naye alikuwa ameacha ratiba Yake yenye shughuli nyingi apate kuja, na hata hawakumkaribisha, walimwacha aketi pale mchafu.

117 "Nanyi mwajua maskini Rabi Levinski alivyosema kule? Alisema. . .Naye mwanamke huyu, aliangalia kule, naye akaja na kumwona ameketi pale, akasema, 'Loo, ni Nani Huyo? Mnajua Huyo ni Nani?'

118 "Ndipo mtu fulani akasema, 'Huyo anadhaniwa kuwa yule nabii. Yeye si nabii, Rabi yule atathibitisha leo ya kwamba yeye si nabii. Hiyo ndiyo sababu akamleta huku chini.'"

119 Mnaweza kukumbuka, wakati mmoja wa jamaa hao anapomwalika Yesu, ana mbinu iliyofichwa mahali fulani, ana mtego hapo mahali fulani. Hakuwa na shughuli yoyote, hakuwa na uhusiano wowote na Yesu, ilikuwa ni kumfanyia njama ama kitu fulani. Kwa hiyo alikuwa amewaalika wengine wote, makuhani waingie, alitaka kuonyesha ya kwamba Yeye hakuwa Nabii. Na kwa hiyo, Yesu akaja hata hivyo. Haidhuru ni kiasi gani Yeye. . .kwamba unajaribu kufanya jambo fulani juu yake, au kujaribu kumwanika, ukimwalika, atakuja, Yeye sikuzote hutimiza miadi Yake; hakosi kamwe.

120 "Kwa hiyo Huyo hapo, Huyo hapo ameketi mle ndani usiku huo. . . siku ile. Ndipo—ndipo maskini mwanamke huyu akasema, 'Ikiwa Huyo Ndiye aliye, Huyo ndiye Mtu huyo, ninaamini Yeye ni Nabii, Naye alikuwa Ndiye aliyemsamehe Mariamu Magdalene, yule mwanamke mbaya kama mimi, akamsamehe dhambi zake.'

121 "Huyo akashuka kwenda mjini, akipanda maskini kichochoro kidogo, kisha akapanda vipandio vichache vinavyokereza kwenye maskini kibanda kidogo cha kale, akafika huko chini na kutoa pesa kidogo alizokuwa amekusanya kwa maisha yake mabaya. Akauchomoa huu, mkoba huu wa pesa, na akasema, 'Siwezi kulitekeleza. Yeye, Yeye ni Nabii, Naye angejua jinsi nilivyopata pesa hizi. Angeweza. . . Lakini ndiyo tu ninayoweza kufanya, ndiyo yote niliyo nayo, na sina budi kumwona, mimi ni mwenye dhambi, sina budi kumwomba anisamehe.'

122 "Huyo akapanda barabarani na kununua kibweta cha marhamu. Akajipenyeza mkutanoni; sijui jinsi alivyopata kufika pale, naye akatazama, na hapo ameketi Yesu. Basi alipofika Kwake, moyo wake ulianza kudunda alipomtazama. Naye akaanguka miguuni Pake akatazama juu, naye alikuwa mwenye dhambi sana hata machozi yakaanza kutiririka usoni mwake, kuitawadha miguu Yake, mwajua. Na—naye angeweza. . . alikuwa akijaribu kuyafuta, aliogopa sana alikuwa akifanya kitu kibaya. Angejaribu kuyafuta, na kisha akaanza *kubusu*, *kubusu*, na kuibusu miguu Yake, na kutazama juu, huku machozi yanatiririka. Angenyosha mikono na kushika nywele zake, naye alikuwa akiipangusa namna hiyo. Ndipo akavunja hicho kibweta cha marhamu, na kuipaka, akilia kwa maana alijua alikuwa mwenye dhambi. Nanyi mwajua, alifikiria. . . "

123 Kama Yesu angaliusogeza mguu, angetoka hapo mbio. Lakini mnaona, haijalishi ni nini, ukijaribu kumhudumia, Yeye atakuruhusu uifanye, anapenda wewe, umhudumie.

124 "Nami ninaweza tu kumwona amesimama pale akimtazama. Naye, akiosha miguu yake, na kulia, 'Najua mimi ni mwenye dhambi. Sistahili kufanya hivi, lakini, Bwana, siwezi kuvumilia kukuona umeketi hapo, na miguu Yako yote ikiwa michafu na inanuka namna hii, sio sawa,' akiosha miguu Yake namna hiyo, kwa mpagao.

125 "Ndipo maskini yule Farisayo, maskini *mwenye kujigamba*, akageuka, akalipuka, akasema, 'Huh-huh-huh! Hmm. Loo, kama angalikuwa nabii, angalijua ni mwanamke wa namna gani alikuwa akiosha miguu Yake, kama angalikuwa nabii. Hilo linathibitisha kwamba yeye si nabii.' Yesu alitulia tu mpaka hatimaye mwanamke huyo akamaliza huduma yake." Hivyo ndivyo anavyokufanyia wewe au mimi, endelea ufanye huduma yako. "Ndipo alipomaliza, Yeye alisimama tu

na kumwangalia, naye akainuka tena. Atasema nini? Yeye hakumwambia, aligeuka, akamtazama yule Farisayo, akasema, 'Simoni, nina neno nitakalo kukuambia: Ulinialika huku, nami nikaja, lakini nilipokuja, hukunipa maji kwa ajili ya miguu Yangu; hukupaka kichwa Changu kilichokauka marhamu; hukunibusu.'" Unapopewa...busu la Kipalestina shingoni, umekaribishwa. "Karibu ndani." Wewe ni ndugu. Unaweza kwenda kwenye sanduku la barafu, upate kitu cha kula, na kuvua viatu vyako, na kulala chini kwenye kitanda cha sofa, na kufanya utakacho, uko nyumbani, wanapokupa busu la makaribisho. Bali akasema, "'Wewe hukunikaribisha kwa busu.'

126 "'Lakini mwanamke huyu,' akamgeukia, kasema, 'mwanamke huyu, tangu nimekuwa humu, tangu alipoingia, hajaacha kuibusu miguu Yangu, na kuiosha kwa machozi ya macho yake.'" Maji ya kupendeza jinsi gani, machozi ya toba, kumtumikia Yeye. Loo! "'Hajaacha kuiosha miguu Yangu kwa machozi yake, ameibusu miguu Yangu, si shingo Yangu, miguu Yangu, tangu nimeingia hapa.'

127 "Naye mwanamke anashangaa atasema nini, kinywa chake kimejaa marhamu, macho yake makubwa ya kahawia yako wazi, nywele zake zimening'inia chini, ninii...uso wake sasa umechachawika, naye anashangaa. Kisha anageuka na kumtazama." Sasa, aone kama Yeye ni Nabii ama siye. "'Nami namwambia, kwamba dhambi zake, ambazo ni nyingi, amesamehewa zote.'" Hilo ndilo ninalotaka kumsikia akisema. "Dhambi zake, ambazo zilikuwa nyingi, zote zimesamehewa." Amina! Je, alikuwa Nabii?

128 Mmoja akasema, "Mnakumbuka," mwingine akainuka, pale juu, kasema, "Je, mnakumbuka pia, ya kwamba alipopitia langoni siku ile, akitoka Yeriko? Kulikuwa na kipofu mmoja aliyeketi pale, naye alikuwa, kasema alikuwa akizungumza, jina lake aliitwa Bartimayo. Mnaukumbuka ushuhuda wake?"

"Naam."

129 "Alisema umati wa watu ulianza kupiga kelele nyingi, naye akasema, 'Hizo kelele zote ni za nini?' na watu wakimkanyaga." Mnajua, bado Yesu ajapo, kelele nyingi. "Na kulikuwa na... Naweza...A—alisema angesikia mshauri mkubwa, mkuu, kiongozi wa chama cha wahudumu akishuka kuja pale kukomesha uamsho huo, 'Hawawezi kuwa na uamsho kama huo hapa chini.' Na kwa hiyo walikuwa wakimfukuza mjini.

130 "Ndipo wakaja mbio na kusema, 'Haya, tumesikia kwamba ulimfufua mtu kutoka kwa wafu anayeitwa Lazaro. Tuna eneo zima la makaburi lililojaa hao hapa juu, njoo ukawafufue, tutakuamini.'" Mnaona, lakini Mungu hamfanyii vitimbi mtu yeyote.

131 Kuna wakati kulikuwa na kundi lingine lililoamini kuwa Yeye hakuwa Nabii. Wakamfunga kitambaa usoni Mwake

barazani mwa Warumi, kisha wakatwaa fimbo, na kitambaa usoni Mwake, wakampiga kichwani, na kusema, “Ikiwa Wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga. Tutakuamini, tuambie ni nani aliyekupiga.” Lakini kamwe hakufungua kinywa Chake na kusema Neno. Bila shaka alijua ni nani aliyefanya jambo hilo, lakini Yeye hamfanyii ibilisi vitimbi, Yeye hufanya tu mambo apate kumtukuza Baba. Hilo ni jambo lile lile. . .Naam. “Ikiwa wewe ni nabii. . . ” Wote walilitilia shaka. Hiyo ni kweli. Wote walilitilia shaka.

132 Zakayo alisema alilitilia shaka, lakini hata hivyo alikuwa mwaminio. Akawa mfuasi wa Kanisa la Full Gospel, Ndugu, naye alikuwa mwaminifu sana kwake huko chini, sababu aliamini ya kwamba Yeye alikuwa Nabii.

133 “Ndipo tunamwona maskini yule kipofu Bartimayo amesimama pale nje, naye. . .msichana fulani akapitia hapo. Naye kabisa alikuwa. . .alikuwa amerushwa upande mmoja, naye akamnyanyua, akasema, ‘Bwana, kuna nini?’

“Akasema, ‘Ewe msichana, naomba uniambie, ni Nani anayepita?’

“‘Loo, kwani hujui? Wewe ni Myahudi, wala hujui siku na saa tunayoishi?’

“‘La, msichana wangu mwema. Sijui angekuwa Nani.’

“‘Mimi ni mwanafunzi Wake.’

“‘Yeye ni nani?’

“‘Yeye ni Yesu wa Nazareti.’

“‘Sijawahi kusikia habari Zake.’

“‘Mbona, Yeye ndiye Nabii wa Galilaya ambaye Maandiko yalinena juu yake.’

“‘Loo, yule Masihi, Mwana wa Daudi?’

“‘Naam.’

“‘Yuko wapi?’

134 Sasa, kama umewahi kuwa Yeriko, tia alama mahali—mahali kipofu Bartimayo alipokuwa ameketi, kisha utie alama mahali Yesu alipokuwa pale alipomsikia. Isingewezekana Kwake kumsikia wakati mmoja anasema, “Salamu kwa Nabii! Utukufu kwa Mungu aliye juu sana!” Wengine walimuunga mkono, mwingine akasema, “Mwondoeni mjini, yeye ni nabii wa uongo! Wafufue wafu, tuonyeshe jambo fulani hapa!” Umati uliochanganyikana. Usingeweza. . .Asingeweza kusikia, sauti yake ya kawaida, asingeweza kuisikia.

Lakini maskini kipofu Bartimayo akapiga magoti na kusema, “Ee Yehova Mungu. . . ”

135 Basi alipofanya hivyo, Yesu akasimama kimya. Laiti ningaliweza kuhubiri juu ya hilo: *Ndipo Yesu Akasimama*

*Kimya*. Alisimama kimya na kusema, “Mleteni hapa.” Imani yake, imani ya yule ombaomba kipofu ilimsimamisha Mwana wa Mungu akiwa njiani kuelekea Yerusalemu na dhambi ya ulimwengu wote imewekwa juu Yake, akielekea Kalvari kusulubiwa. Ndipo imani ya ombaomba mmoja, akiwa magotini mwake, akilia kwa sauti, imani yake, Yeye akaihisi imani yake. Hakika Yeye alikuwa Nabii wa Mungu.

136 Loo, ni mkutano wa ushuhuda jinsi gani! Laiti tungelikuwa na wakati wa kuendelea, lakini hatuna, hatuna budi kusimamisha mkutano wa ushuhuda na kufunga. Loo, labda inakaribia kuchelewa kidogo, na tayari giza limeingia. Loo, maskini ile mashua ya kale ilikuwa ikiyumbayumba tu, kutoka upande mmoja hadi mwingine, wakipiga kelele, “Utukufu! Haleluya!” Loo, waliridhika! Walijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi.

137 Yapata wakati huo, kule nyuma ya vilima huko Galilaya, ibilisi akainuka. Akasema, “Uh-huh. Nimewapata mahali ninapowataka hasa, wameondoka bila Yeye. Sasa, nitawapata.”

138 Nami nashangaa, ndugu, kama makanisa yetu hayajafanya jambo lile lile. Katika msisimko wa uamsho, tunajaribu kuona ni nani anayeweza kuwa na kanisa kubwa zaidi, na madhehebu yaliyovalia vizuri zaidi, kusanyiko lililovalia vizuri zaidi, hasa, na madhehebu makubwa zaidi, washiriki wengi zaidi. Nashangaa ikiwa hatujateleza na kwenda kando katika haya yote bila Yeye. Mnaona? Kumwacha nyuma, amelala, kwa sababu tu wa—wana umati bora, na kanisa kubwa zaidi. Na hapo—hapo ndipo hofu yangu inapoingilia kwa ajili ya kanisa langu la Kipentekoste ambalo nina bidii nalo, kwamba litakikosa kile Kiini halisi, ule Ufalme halisi wa Mungu. Kumbuka, ndugu, dada, Pentekoste si dhehebu. Pentekoste ni tukio, Wamethodisti, Wabaptisti, Waanglikana, yeyote atakaye. Pentekoste, huwezi kuundia Pentekoste dhehebu, maana huyo ni Roho Mtakatifu. Unaona? Wala huwezi. . .Ni tukio linalowajia watu wote.

139 Ndiposa wakamwona. Walikuwa wameenda bila Yeye, kwa hiyo akasema, “Hii hapa nafasi yangu ya kuwazamisha.” Kwa hiyo akaanza kupulizia pumzi yake ya sumu. Whiu. Hiyo bahari kubwa ikaanza. . .Kasema, “Nitawazamisha huko nje katikati ya bahari sasa. Nimewafikisha pale ambapo hawawezi kujisaidia.” Whiu. Wimbi baada ya wimbi!

140 Anasema nini siku hizi kwa wimbi lake baada ya wimbi? “Siku za miujiza zimepita.” Whiu. “Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Ninyi watu wa Kipentekoste hampaswi kuanza na hilo. Mnapaswa kujiunga na makanisa makubwa ya kiekumeni. Mnapaswa—mnapaswa kuingia katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni.” Whiu. Mawimbi ya shaka yakielea kupitia kanisani.

141 Na jambo la kwanza maskini—maskini mtumbwi wao ukajaa maji. Nguzo ya matanga ikavunjika, makasia yakavunjika, maskini. . . Mnajua maana ya kuwa na mashua iliyojaa maji, iko tayari kuzama hata chini. Nayo hiyo hapo, matumaini yote yalikuwa yametoweka. Maskini . . . Ilibidi tu kuiacha ielee.

142 Lile wimbi, huku ibilisi ameketi juu ya kila wimbi, akisema, “Hah! Tutawapata kwenye linalofuata. Tutawazamisha wakati huo mwingine. Wao ni wanafunzi wa Kristo. Tutawazamisha kwa sababu wameondoka, walimwogopa Yeye, wakaondoka. Kwa hivyo sasa, tuta—tuta—tuta—tutampata, tutawapata.” Nao hao hapo, wakienda huku na huko, huku ibilisi akisema, “Nitawazamisha baada ya hili.”

143 Lakini mwajua nini? Walipoondoka, Yeye hakuwaacha; alipanda kilima kirefu kuliko vyote nchini apate kuwatazama, kuwaangalia walipokuwa wakienda. Nanyi mwajua, alipokufa kule nyuma Kalvari, kamwe Yeye hakutuacha, alifufuka tena, akapaa juu, juu, kati ya Mirihi, Jupita, Zuhura, mbali kupita mwezi, nyota, Njia ya Kilimia Cheupe, akaingia Mbinguni, kisha akapita Mbingu kwa mbali sana. Biblia ilisema alipaa juu. Hata Mbingu ni mahali pa kuweka miguu Yake. Kwa nini? Kadiri unavyopanda juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali. Na jicho Lake liko kwenye shomoro, na ninajua Yeye anatazama sasa hivi. Shida ilipokuja, Yeye aliwaona katika shida, na muda si muda wajua, Huyu hapa akaja akiwaendea juu ya bahari, akitembea. Basi sehemu ya kusikitisha ya hadithi hii ni hivi, hii papa hapa ndiyo sehemu ya kusikitisha zaidi. Walikuwa karibu kuzama.

144 Na kama makanisa yetu hayatarudi kwenye uamsho tena, yamrudie Roho Mtakatifu, warudi, na wasiendelee kusonga mbele kwenye mkondo huo kama vile makanisa ya kimadhehebu yanavyoenda, tutazama. Hiyo ni kweli. Tunarudi moja kwa moja, kwa sababu kila kanisa lililopata kuunda dhehebu, Mungu aliwaweka kwenye rafu. Nami nataka mwanahistoria yeyote aniambie ni wapi liliwahi kuinuka tena, hakuna kamwe katika historia lilipowahi kuinuka, nami nimesoma Baraza la Nikea, Baraza Lililotangulia Nikea, *Wazee wa Nikea*, *Babeli Mbili* cha Hislop, *Enzi za Mwanzoni* cha Pember. Loo, kamwe hakuna mahali ambapo kanisa liliwahi kuunda dhehebu, ila ambapo Mungu aliliweka kwenye rafu, wala hakulitumia tena, kisha akachukua kitu kingine, na kuendelea nacho. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. “Mungu anaweza kutoka kwa mawe haya . . . ” Hapo ndipo shida yetu ilipo usiku wa leo. Usiku wa leo iko hapo.

145 Na huyu hapa Yesu anakuja akitembea juu ya bahari, nao walidhani Yeye alikuwa ni mzuka, walimwogopa. Wakasema, “Loo!” Wakapiga kelele, “Loo, inaonekana kama mzuka! Ninahofu ni kivuli!” Kitu pekee ambacho kingeweza kuwaokoa, walikiogopa.

146 Sasa, kaeni kimya kabisa. Jambo lile lile linafanyika. Popote

uendapo, nao wanamwona Roho Mtakatifu akipambanua, yale hasa aliyosema, akithibitisha kwamba Yeye ndiye Masihi akitenda kazi ndani ya watu Wake, watu wanasema, “Ni telepathia. Vema, jamaa huyo ni mpiga ramli.” Mnaona? Kitu kile kile walichokiita hiyo. Mnaona? Kitu pekee kinachoweza kuwaokoa, wanakiogopa. Hiyo ni kweli.

147 Lakini Yesu alisema nini? Yeye alisema, “Msiogope; changamkeni; ni Mimi.” Amina. “Msiogope; ni Mimi; msiogope.” Na aseme hivyo mioyoni mwetu usiku wa leo, enyi marafiki.

148 Nasi tunaposhuka kupitia mstari huu wa maombi, hebu tukumbuke, “Msiogope.” Sasa, kama mna ushirikina kidogo, mashaka kidogo mioyoni mwenu. . . Samahani kwa kuyachanganyisha maneno yangu. Hii ni mikutano kumi na mmoja mfululizo kwangu na karibu upambanuzi elfu moja mia tano katika miezi miwili iliyopita. Karibu nimekwisha. Nina siku zingine tatu usiku, nami sina budi kupumzika kidogo, la sivyo siwezi kukaa hapa. Kila kitu. . . Ninaketi na kuzungumza na watu, inaonekana kana kwamba bado, ni ono. Mnaona? Mimi. . . Ndiyo sababu ni—nimechoka. Hamtambui ninayopitia. Lakini sina budi kufanya kazi, jua litashuka hivi karibuni, wala hakutakuwako na Nuru tena, kutakuwa giza wakati huo.

149 Wanasema ukomunisti utautawala ulimwengu. Kamwe msiamini hilo. Ukomunisti hautafanya lolote. Nionyeshe mahali pamoja katika Biblia ambapo ukomunisti utawahi kutawala. Biblia inasema Urumi utachukua madaraka, sio ukomunisti, angalieni maono ya Danieli. Mnaona? Sio—sio ukomunisti, ni kibaraka mikononi mwa Mungu cha kuangamiza Urumi. Lakini Urumi, ninyi uogopeni huo, sio ukomunisti, huo si kitu, huo ni bure. Ila, mnasikia kuhusu Urusi, ukomunisti wote, nimekuwa kule, nikaona baadhi ya watu wazuri sana niliopata kuwaona maishani mwangu. Kuna asilimia moja tu ya Urusi nzima ambayo ni ya kikomunisti. Kile Urusi inachohitaji. . . Waliona udhaifu wa kanisa Katoliki, na jinsi walivyofanya, wala hawakufanya lolote, na kuchukua fedha zote kutoka humo nchini, ndipo wakageuka kuwa komunisti. Hiyo ni kweli kabisa. Lilipaswa kushikilia kiwango hicho.

150 Urusi inahitaji uamsho. Wakati mvulana huyo mdogo alipofufuliwa katika wafu, kule Ufini, nilisimama kule pamoja na mamia ya askari hao wa kikomunisti, pamoja na saluti hiyo ya kikomunisti, huku machozi yakitiririka mashavuni mwao. Wakati hilo liliposambaa nchini kote, wao walisema, “Tutampokea Mungu anayeweza kuwafufua wafu.” Naam, bwana. Hakika. Wanataka ninii. . . Wanahitaji uamsho.

151 Tunachohitaji ni mmoja. . . Mungu anahitaji mtu mmoja tu ambaye anaweza kumweka katika udhibiti Wake, huyo tu ndiye anayemhitaji. Ndugu, Kristo yuko hapa usiku wa leo, usiogope hilo, ni Kristo. Unapopitia kwenye mstari huu, kumbuka

tu hili ya kwamba ni Kristo. Nitalisimamisha kusanyiko na kuwaombea; nitakuwa na ndugu zangu wahudumu hapa wanaoamini katika uponyaji wa Kiungu, washuke waje.

152 Mara nyingi watu. . .Mhudumu ataingia mjini, na labda ana imani sana, naye ata—atafanya mazungumzo yote, na kuwaombea wagonjwa wote, na hata kuwabatiza watu. Ndipo inakuwaje? Ndipo huyo mwinjilisti anapoondoka, maskini huyo mchungaji anaonekana kana kwamba ameketishwa kwenye safu ya nyuma huku yeye si lolote, hata hivyo, huyo ndiye mchungaji wenu, huyo ndiye mtu aliyewafikisha umbali huu, mwaminini. Nami ninawatakeni ninyi nyote mjue, sio lazima mngojee mpaka karama fulani maalum zitokee. Ikiwa una haja ya mambo yoyote ya kiroho, mtake ushauri mchungaji wako, ndiye aliyekuongoza salama umbali huu, atakupeleka mbele, hiyo ni kweli, mtumishi wa Mungu.

153 Nami nawatakeni mjue, hivi majuzi usiku, nilisimama kwenye mstari wa yapata wachungaji thelathini ama arobaini, nami nikaruka hadi mwisho huo mwingine wa mstari na kuwachukua watu namna hiyo, na asilimia kubwa, kubwa zaidi yao waliponywa kabla hawajafika mahali nilipokuwa nimesimama. Hao wachungaji waliojazwa na Roho Mtakatifu, wakiwawekea mikono yao, hao walikuwa ni Wamethodisti, Wabaptisti, na Wapentekoste, na wote pamoja, walikuwa wakiamini. Walikuwa na Roho Mtakatifu, nao walikuwa wakiamini, hiyo ni kweli, na walikuwa wakiitekeleza hiyo kazi. Hiyo ni kweli.

154 Wala msiogope upambanuzi huu, Mungu aliuahidi. Na maskini siku hizi chache usiku, mnaamini hivyo? Mwaminini Mungu. Na tuombe sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu. Sasa, tunajiandaa kufunga. Katika dakika ishirini hadi thelathini zijazo tutakuwa tunaambiana kwaheri.

155 Na kama nikirudi mwaka ujao, kuna baadhi yetu hawatakuwa hapa, mnajua hilo. Kama. . .Huenda hata mimi mwenyewe nisiwe hapa; wewe unaweza usiwe hapa. Huu utakuwa ndio mkutano wetu wa mwisho katika dunia hii, ndipo hatuna budi kukutana tena, hiyo itakuwa kwenye ile Hukumu, ama Kiti cha Hukumu cha Kristo. Utakuwa umesimama huko ama umehesabiwa haki au bila kuhesabiwa haki. Utakuwa umechelewa sana basi, huwezi kufanya chochote kulihusu. Nanyi mnajua na kuamini, ya kwamba Mungu kupitia Biblia Yake, hapa, amethibitisha tena na tena ya kwamba Uwepo Wake uko hapa.

156 Hivi wewe si Mkristo? Sitakuomba, uje kwenye madhabahu yoyote, nitakuuliza tu swali, nataka unijibu kutoka moyoni mwako. Ikiwa wewe si Mkristo nawe unataka nikuombee uwe Mkristo, waweza tu kuinua mkono wako huku kila mtu ameinamisha kichwa chake? Useme, "Niombee, Ndugu

Branham, sivyo nilivyo." Mungu akubariki, mama. Baadhi . . . Mungu akubariki. Mwingine? Sema . . . Mungu akubariki, mama. Na Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, hapa. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, kijana mwanamume. Mungu akubariki.

157 "Mimi si Mkristo, nataka kuwa Mkristo, ninainua mkono wangu." Mungu akubariki, hapo nyuma, bwana. Sasa, kumbukeni, nisingaliuliza swali hili kama Roho Mtakatifu tayari hakunigusa. Hiyo ndiyo sababu nilianza na ujumbe. Je, mliona ile sauti tofauti nilipofikia kuosha miguu ya mwanamke huyo, ama, kuosha miguu ya Yesu, yule mwanamke? Nuru hiyo iliruka moja kwa moja juu yangu, imesimama papa hapa, mbele yangu sasa. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu, ninafanya tu vile Yeye anavyoniambia, "Waambie wainue mikono yao."

158 Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, naam. Ninauona mkono wako. Mtu mwingine? Mungu akubariki. "Unirehemu, Mungu, na—nataka kuokoka." Mungu akubariki, mama. "Ninataka kufanya . . . Nataka kuokoka na kumtumikia Yesu. U—ulimwengu unammwagia uchafu tena, kinyaa cha ulimwengu. Wanamwita 'mtakatifu anayejibingirisha.' Wanawaita kundi la watu wenye kichaa. Nataka kuchukua msimamo wangu, na kwa maisha yangu, ya kwamba nitaishi mtakatifu mbele ya ulimwengu huu, ninataka kuosha uchafu kutoka miguuni Mwake. Ukosoaji wanaolipa Kanisa Lake takatifu, nataka kuosha huo uchafu kutoka miguuni Mwake kwa machozi yangu ya toba." Mungu akubariki, mwanangu. Mungu akubariki. Mungu akubariki, mama. Hilo ni jema.

159 Loo, naona wazungu wengi wameinua mikono yao. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Ubarikiwe. Hilo ni zuri sana. Aminini tu. Yote yanawezekana kwa hao waaminio. Iweni tu na imani. Vema.

160 Baba wa Mbinguni, uliiona mikono hiyo. Mimi ni . . . Kama mtumishi Wako ninawadai. Ninawadai watu hawa wa thamani, baadhi yao sitawaona tena. Lakini, Mungu, walivunja kanuni zote za kisayansi papo hapo, wakainua mikono yao. Sasa, kulingana na sayansi, mikono yetu haina budi kuning'inia chini; nguvu za uvutano zinaishikilia ardhini. Lakini inaonyesha kwamba wana roho ndani yao inayoweza kufanya maamuzi, nao wanainua mikono yao kwa Muumba wao, ikionyesha kwamba roho fulani ndani yao, na kuna Mmoja huko nje anayesema nao, nao wanamjibu Roho huyo, ambaye ni Roho Mtakatifu.

161 Pia, Yesu, ninataka kunukuu Maneno Yako. Mbingu na nchi zitapita, lakini Hayo hayatapita. Ulisema katika Maandiko ya Biblia iliyobarikiwa katika Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu," nami nimeinukuu tu Biblia Yako usiku wa leo, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na

kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Uliahidi jambo hilo, Bwana. Wameinua mikono yao, wanakuamini, wanamwamini Yeye aliyekupeleka, wanalikubali Neno, nami ninawadai. Wala Shetani hawezi kuwakaribia tena. Na—nawadai kwa ajili ya Injili.

162 Naye Yesu anawakabidhi kwa Baba Yake kama thawabu ya upendo, "Wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya mkononi mwa Baba Yangu." Wao ni Wako, Bwana. Ni—ninawaamini, ya kwamba wataenda kwenye kanisa la Kikristo mahali fulani, kanisa zuri la Injili kamili, na kubatizwa kwa ubatizo wa Kikristo, na kumpokea Roho Mtakatifu. Ndipo ukungu wa mauti unapoanza kuelea usoni mwao, moja ya asubuhi hizi, wakati moyo wao utakaposimama, ile meli ya kale ya Sayuni itakuja kuwachukua abiria wake na kuwashusha salama huko Ng'ambo. Tujalie, Bwana. Ninaamini, nikitumaini katika Jina la Yesu. Amina.

163 Ninamwamini. Mnamwamini? Sasa, kila mmoja uliyeinua mikono yako...Sasa, ninaamini katika kufanya miito ya madhabahuni, hakika ninaamini. Lakini ninii halisi...Hilo si la kimitume. Biblia ilisema, "Wote walioamini walibatizwa." Mnaona? Mikutano ya maombi imekuwa...Hakika, tulianza kufanya miito ya madhabahuni, tukija na kuomba katika siku za Wamethodisti, kanisa la mwanzoni huko Uingereza, walipoidhinisha shule ya Jumapili, na kadhalika, lakini hiyo ni—hiyo ni sawa. Ninaamini katika Wakristo kuja madhabahuni wakiomba, ninyi wenye dhambi, na kadhalika. Lakini sasa hivi...Mnaona? Hakuna nafasi yoyote, vyombo na kila kitu hapa. Lakini ninaamini kwamba ulimaanisha hilo, na kama hukumaanisha, haitakusaidia kwa vyovyote vile. Unaona? Lakini kama ulilimaanisha, umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Ndivyo alivyosema. Hiyo ni kweli, ulilimaanisha. Kuna mikono thelathini au arobaini.

164 Sasa, mnawaona wachungaji hawa hapa? Hao ni ndugu zenu, hudhurieni kanisa lao mkabatizwe. Na hebu...Waulize kuhusu vile, jinsi ya kumpokea Roho Mtakatifu, watakuelekeza, jinsi ya kufanya hivyo. Sasa, tunapowaombea, ninataka kuhakikisha ya kwamba Roho wa Mungu yuko juu yetu. Vema.

165 Nataka kuwaulizeni: Je, mnaamini? Mnaona ile picha kule, ile Nguzo ya Moto iliyo kwenye picha? Mmeiona. Sasa, nimeiona Hiyo tangu nilipokuwa mvulana mdogo, iko kote katika kumbukumbu. Mara ya kwanza ambapo iliwahi kupigwa, gazeti la Canada liliichapisha miaka thelathini na mmoja iliyopita, katika jimbo lote la Canada, majimbo yote, milki ya Canada, kasema, "Nuru ya ajabu inaonekana juu ya mhudumu wakati akibatiza mtoni." Hiyo ilikuwa mwaka wa 1930, chini ya Barabara ya Spring huko Jeffersonville, Indiana, wakati

karibu watu elfu kumi walikuwa wamesimama pale, nilikuwa nikimbatiza mtu wangu wa kumi na saba.

166 Nikasema, "Baba wa Mbinguni," nami nilikuwa kijana mhubiri wa Kibaptisti, nami nikasema, "Baba wa Mbinguni, ninaweza tu kumbatiza kwa maji kuwa mshirika wa kanisa hili, lakini ninaomba kwamba utambatiza kwa Roho Mtakatifu."

Niliposema hivyo, Kitu fulani kikasema, "Angalia juu!" Kisha nikaisikia mara ya pi-. . .mara ya tatu ikasema, "Angalia juu!"

167 Nami nikageuka na kuangalia, na ngurumo kubwa ikatetemesha kote juu ya umati, na hii hapa Nuru hiyo inakuja ikitelemka chini, na kusimama moja kwa moja juu yangu mahali nilipokuwa nimesimama. Ndipo Sauti ikatoka Kwake, kasema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia Kuja kwa Kristo Mara ya Kwanza, Ujumbe wako utatangulia kule Kuja Mara ya Pili." Liangalieni leo, uamsho ulizuka baada ya hayo, nao ukaenea ulimwenguni, uamsho wa Kipentekoste, wa Roho Mtakatifu. Sasa, Walutheri, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wakatoliki na wote wanampokea Roho Mtakatifu, kila mahali, nalo Kanisa likijiandaa kuingia. Ujumbe unafika mwisho. Mnaona? Haya basi.

168 Sasa, sote tunajua sasa ya kwamba Malaika wa Agano, hiyo Nguzo ya Moto ilikuwa ni Malaika wa Agano, ambaye alikuwa ni Kristo. Je, mnaamini hilo? Ndugu zenu wataamini hilo, wahudumu, hakika. Mnaona? Alikuwa. . .Musa aliiacha Misri, akihesabu kushutumiwa kwake Kristo kuwa hazina kuu kuliko ile ya Misri. Mnaona? Ilikuwa. . .Sasa, huyo alikuwa ni Kristo katika Nguzo hiyo ya Moto wakati ilipotulia mlimani.

169 Sasa, alipokuja hapa duniani, Yeye alisema, "Nilitoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu." Je, hiyo ni kweli? Na baada ya kufa, kuzikwa, na kufufuka Kwake, baada ya kupaa Kwake, Sauli, ambaye baadaye aliitwa Paulo, alikuwa njiani akishuka kwenda Dameski kuwakamata watu waliokuwa katika njia hii. Na mchana kabisa, Nguzo hiyo kubwa ya Moto ilionekana mbele yake, na kumwangusha chini, na kuyang'oa macho yake. Ndipo Sauti ikasema. . .Sasa, hakuna mtu aliyeona hiyo—hiyo Nguzo ya Moto ila yeye.

170 Je, mnaamini wale Mamajusi waliifuata Nyota? Hakuna kituo cha kuangalilia kilichoiona wala chochote kile, wakiangalia mbingu, kwa jumla. Kamwe hawakuiona, maana hawakuwa wakiitazamia. Mnaona? Anaonekana tu kwa wale anaotaka.

171 Sasa, Sauli alibwagwa chini. Wao—wao—wao hawakuona Nguzo yoyote ya Moto, bali ilikuwa halisi sana kwa Sauli hata ikampofusha. Kisha Sauti ikatoka Kwake, ikasema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Akasema, "U nani Wewe? Ni nani huyu Nguzo ya Moto?"

Akasema, "Mimi ni Yesu. Ninatoka kwa Mungu, ninaenda kwa Mungu."

172 Sasa, Yeye . . . Yote aliyokuwa Mungu aliyamimina ndani ya Kristo. Yeye alikuwa ni Utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Na yote aliyokuwa Kristo, aliyamimina ndani ya Kanisa Lake, "Siku hiyo mtajua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Mnaona? Ni Mungu. Ilikuwa ni Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu. Mnaona ninalomaanisha? Huyo hapo, Mungu yule yule.

173 Sasa, kama Nuru hiyo haifanyi kazi zile zile ilizofanya ilipokuwa katika Mwana wa Mungu, basi si Yeye yule, siye. Lakini ikiwa inafanya kazi zile zile . . . Kama tu nilivyosema, kama ungeweza kuondoa uhai wote kutoka kwa mtofaa, kila sehemu ya huo uhai, na kuuhamisha uhai wa mpea katika mtofaa, ungezaa peasi. Unaona? Kwa sababu huo uhai uko ndani yake. Hayo ndiyo unazaa, tunda liko katika uhai, bila shaka. Na hilo ni jambo lile lile hapa. Ukiweka Uzima wa Kristo, na kuuondoa uhai wa mwenye dhambi, hana budi kufa kwanza, ndiposa Uzima wa Kristo unapoingia ndani yake, basi atazaa Uzima wa Kristo kwa sababu Huo ndio unaoishi ndani yake. Unaona? "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya," maana Uzima Wake uko ndani yake.

174 Sasa, ndugu zenu, wachungaji wenu, huenda wasiweze kutabiri na kubashiri mambo, kwa sababu manabii huzaliwa manabii. Kuna karama ya unabii Kanisani, lakini manabii huzaliwa manabii, daima. Mnaona? Sa—sauti ya unabii mikutanoni, karama ya unabii haina budi kuamuliwa. Lakini angalieni. Sasa, lakini kuna zaidi ya ninii . . . Kuna mitume, manabii, wachungaji, walimu, wainjilisti. Mnaona? Hizo ni ofisi. Na ndugu hawa . . . Mimi si mwalimu, wala mhubiri. Mnaona? Kwa sababu siwezi kushikilia ofisi yao, wao hawawezi kushikilia yangu. Lakini, "Mungu ameweka Kanisani . . . " Hao watu ni watu wa Mungu pia, wana haki sawa tu kumwombea mtu yeyote. Na mimi niko hapa tu . . .

175 Mnaona, sote tuko kama, ili kwamba ndugu zangu Wahindi watalipata, sote tunavua samaki, ndivyo tunavyofanya. Na kuna kiasi *fulani* tu cha samaki katika ziwa hili wanaopaswa kuvuliwa, na ni hao tu. Ufalme wa Mungu ni kama mtu aliyechukua wavu, akaenda, akautupa, huo wavu, akauvuta nje, alikuwa na vyura, mijusi, wadudu, nyoka, na samaki. Vema, kwanza kabisa walikuwa ni samaki, kwanza kabisa walikuwa vyura, kitambo kidogo tu, nao vyura wataruka warudi majini, nao nyoka watarudi mbio, buibui wa majini watarudi nyuma, na kamba watakimbia chini ya kitu fulani, lakini samaki ni wa Bwana.

176 Sasa, hawa ndugu wanavua kwa juya katika sehemu

mbalimbali za ziwa kuu la Mungu. Sasa, nimekuja hapa katika mji huu mdogo kusuka wavu wangu pamoja na wenu, ili tuweze kufikia mbali sana, mbali na kona moja, au, jumuiya moja, kufikia mbali sana, kisha tuvute, ni nyavu zetu zote zikiwekwa pamoja. Je, hamwoni? Sisi ni ndugu. Tunaweza—tunaweza kutokubaliana. Kama nikija na kumwuliza Ndugu Byskal hapa kuhusu theolojia fulani, angeninii...tunaweza tusikubaliane, wala sijawahi kukutana na mtu mzuri zaidi maishani mwangu. Mnaona? Tunaweza tusikubaliane. Lakini...Watoto wangu huko nyuma...Nina watoto watatu nyumbani. Ikinibidi kununua aiskrimu, sina budi kununua za aina tatu mbalimbali, mmoja anataka vanila, mwingine anataka stroberi, na mwingine anataka chokoleti, vema, ninapokuja na aiskrimu, zinaonekana kama upinde wa mvua, lakini angalieni, zote ni aisrimu, ladha haijalishi. Haya basi, ndugu! Utukufu! Hiyo ni kweli. Sisi sote tunakula aiskrimu.

177 "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Na jinsi tunavyoweza kuketi hapa usiku wa leo, upinde wa mvua ni agano. Mungu ni Mungu wa aina mbalimbali. Je, hamwamini hilo? Mungu haweki kila kitu kama Sears and Roebuck, Harmony House. Hapana, bwana, Mungu ni Mungu wa aina mbalimbali. Yeye hufanya milima mikubwa, anafanya milima midogo, anafanya majangwa, anafanya bahari, anafanya watu wadogo, watu wakubwa, anafanya maua meupe, maua meusi, maua ya bluu, maua ya waridi. Yeye ni Mungu wa vitu mbalimbali. Na hivyo ndivyo anavyotaka.

178 Lakini ninii...Sasa, vipi kama ua jeupe linaingiliana na ua jekundu, na kusema, "Huh. Sitakuwa katika hilo shada la Mungu. Hum-um! La, bwana, kwa sababu mimi si...wewe si ua jekundu." Hapana, yanachanganyikana tu kwa ajili ya Bwana wao. Amina. Hivyo ndivyo tunavyofanya, tunachanganyikana kwa ajili ya Bwana wetu. Hiyo ni kweli.

179 Sasa, Roho Mtakatifu yuko hapa, naye Yesu alisema, "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi." Je, hiyo ni kweli? Wasingeweza kumwamini, akiwa Mwanadamu, akiwa Mungu. Wasingeweza tu kuona kwamba hiyo ingeweza kuwa chochote. Kasema, "Unajifanya Mwenyewe kuwa sawa na Mungu, ukiwa Mwana wa Mungu." Sasa, tunajua Yesu alikuwa Mwana. Alisema, "Mwana hawezi kutenda lolote kwa nafsi Yake, ila lile amwonalo Baba analitenda."

Tomaso alisema, "Utuonyeshe Baba na inatutosha."

180 Akasema, "Nimekuwa pamoja nanyi kwa muda mrefu, hamnijui Mimi? Yeye aliyeniona Mimi amemwona Baba. Si Mimi nizitendaye kazi. Ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu." Mungu ni Roho; Yesu alikuwa Mwanadamu, Yeye alikuwa ni Maskani ambayo Mungu aliishi ndani yake. Mnaona?

181 Sasa, Yeye alikuwa na Roho bila kipimo, kama vile maji hayo yote kule baharini, hayo Ndiyo yaliyokuwa ndani Yake. Lakini ndani yetu, ni kijiko kimoja tu kutoka Kwake, tunaye kwa kipimo. Lakini kumbukeni, kemikali zile zile zilizo katika bahari nzima ziko kwenye hicho kijiko, sio nyingi hivyo, lakini aina ile ile. Amina. Mnaona? Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya."

182 Sasa, wakati alipoonyesha ishara Yake ya Kimasihi, hiyo ilikuwa kwa ajili ya watu fulani. Yeye alikuwa ni mwalimu, "*Haya* hapa, haya hapa mambo mbalimbali," yote aliyofanya. Hapa yanawakilishwa katika Kanisa Lake. Yeye yuko hapa kuwasaidia, nasi tuko hapa tukilihubiri Neno, tukifanya kila tuwezalo kuwasaidia.

183 Sasa, kama nimesema kweli, Mungu anawajibikia Ukweli Wake. Hiyo ni kweli? Sasa, kabla hatujaja hapa juu... Nanyi mnajua, wachungaji wenu, mnajua wao ni walimu, mnajua hao ni watu hodari wa Mungu katika Neno. Na sasa, ili Mungu aweze kusema kama nimesema kweli ama la, ni wangapi humu ndani sasa walio wagonjwa? Inueni mikono yenu. Kabla hatujaomba, inua tu mkono wako, useme, "Mimi ni mgonjwa, nataka uniombee." Vema. Sasa, kuna mikono ya kila namna, bila shaka nisingejua upi ni upi. Sasa, hebu tuombe tu mioyoni mwetu.

184 Sasa, Biblia ilisema kwamba Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Kama hiyo ni kweli sema, "Amina." Sasa hivi Yeye ni Kuhani Mkuu. Na kama ulimgusa, nayo Waebrania 13:8 ilisema, "Ni yeye yule jana, leo na hata milele," Angetenda vivyo hivyo. Mnaona? Yuko katika umbo la Roho Mtakatifu. Basi kama—kama ukigusa vazi Lake, kama mwanamke yule alivyofanya, kwa mambo ya udhaifu wako, basi atakujibu moja kwa moja, maana hii hapa sehemu ya Kanisa Lake, hawa hapa walimu, na vituo, na njia. Mnaona? Basi angalieni tu kama si Mungu. Hebu watu humu ndani wajue ya kwamba Yeye ni Mungu. Yeye ni Mungu, na anabaki yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa, na tuombe kwa kimyakimya, kila mmoja, kwa ajili ya magonjwa yetu. Hebu, kila mtu, kwa njia yako mwenyewe uombe. Amini tu. Useme, "Mungu, unirehemu, nijalie niguse vazi Lako, Baba. Ninaungama dhambi zangu, nimekosea. Na Bwana Mungu, kama tu utajalia—utajalia..."

185 Nanyi watu huko nyuma, mlimkubali hivi punde tu, mkisema, "Bwana, mtu huyo hakika alijua kulikuwa na wenye dhambi humu ndani la sivyo asingetoa wito kama huo, nami nikainua mikono yangu. Sijawahi kuona kitu kama hiki kikifanyika. Nilimsikia akisimulia mkutano huo wa ushuhuda. Kama ninaweza kuuona ukifanywa, nitaanzisha mkutano wa ushuhuda pia, kwamba niliuona ukifanywa, kwa sababu

walisema Wewe ni yeye yule." Sasa, wewe omba na kusema, "Baba, niruhusu niguse vazi Lako. Katika Jina la Yesu. Amina."

186 Sasa, angalieni huku. Aminini. Hebu twende tu kwa—kwa sehemu ili niweze kuizingatia hiyo sehemu. Sasa, wewe amini kwa moyo wako wote. Sasa, hebu Roho Mtakatifu . . . Kwa uchaji sasa, kila mtu awe na uchaji na mtulivu uwezavyo kuwa. Wala kamwe msininii . . . Angalieni—niangalieni mimi, lakini msininii . . . Kama vile Petro na Yohana walivyopita langoni, wakasema, "Tutazame sisi." Hiyo ilimaanisha, azingatie walichokuwa wanasema. Akasema, "Mimi sina fedha wala dhahabu; nilicho nacho ndicho nitakupa."

187 Sasa, kama ningeweza kumponya yeyote wenu, ningekuja nifanye hivyo, mnajua hilo, ninaamini mnaamini hilo, kama ningeweza kufanya hivyo, lakini siwezi, hakuna mtu mwingine awezaye. Hata Mungu hawezi, tayari ameshafanya hivyo. Jambo pekee, Yeye hukujulisha ya kwamba Yuko hapa kuthibitisha aliyosema yalikuwa sahihi. Ni wangapi wanaelewa hilo? Kwamba Uwepo Wake unathibitisha kwamba . . .

188 Angalieni hapa. Mbona, lingekuwa ni jambo kubwa zaidi jinsi gani ku—kumwona m—mtu huko nje ambaye hujawahi kumwona maishani mwako, na kuwafunulia maisha yao, ama kitu kama hicho kwao, wakati ingekuwa, hata kuwawekea tu mikono wagonjwa, na kuwaona wakipona? Ni mwujiza ambao hatujakuwa nao Kanisani kwa miaka elfu mbili. Lakini iliahidiwa wakati wa jioni, na sisi hapa, si kwa kanisa la kawaida, bali kwa Kanisa teule, Uzao wa Ibrahimu, pekee. Sasa, aminini.

Kama mtu yeyote haamini kuwa ni Mungu, njoo hapa ukachukue mahali pangu. Iweni na imani.

189 Kuna msichana mdogo, mrembo anayeketi papa hapa akinitazama, na maskini . . . ni msichana mdogo wa Kihindi. Una shida fulani, Dada. Na ndani ya maskini moyo wako wa kitoto, uligusa Kitu fulani. Ninataka kukuuliza jambo fulani, Dada. Ulihisi hisia tamu sana ikikuzunguka, mara tu nilipozungumza, sivyo? Nuru hiyo ilikuja moja kwa moja juu yako. Unasumbuliwa na ukurutu ambao ni sugu. Hiyo ni kweli, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Utakuacha sasa. Unaona? Imani yako inafanya hivyo. Mpenzi, ulikuwa na kadi ya maombi? U—ulikuwa na moja, haitakubidi kuitumia sasa. Niliangalia chini, nikadhani niliona moja, alikuwa na kitu mkononi mwake. Iweni tu na kicho.

190 Huyu hapa, mwanamke mzungu, ameketi huko nyuma akinitazama. Anasumbuliwa na kitu kibaya kooni na kifuani mwake. Mungu, usimwache aukose. Baba wa Mbinguni, msaidie, tafadhali. Binti Alexandra, amini kwa moyo wako wote. Unaamini? Inua mkono wako. Vema. Sikiliza, sikiliza hili. Nilipozungumza kwa mara ya kwanza, ulifikiri ilikuwa ni wewe,

lakini hukuwa na uhakika. Hiyo ni kweli. Kisha ukafadhaika sana, ukashikwa na hofu. Nuru hiyo ilimwacha kisha ikarudi. Mnaona? Ndipo iliporudi, nilimwona ameshika kitu mkononi mwake akitoka posta, nacho kikasema, "Alexandra." Vema. Endelea mbele. Imani yako inakuokoa. Amina. Unamwamini? Hiyo ndiyo yote unayopaswa kufanya ni kumwomba na kupokea.

191 Vipi kuhusu mtu fulani *hapa* ndani? Hapa. Huyu hapa mtu ambaye kidogo ana . . . yuko kati ya umri wa makamu na umri wa uzeeni. Ananiangalia moja kwa moja, anashangaa moyoni mwake, kama kweli ninazungumza na yeye. Ni wewe. Unasumbuliwa na kitu fulani usoni mwako, kama mshipa unaokufa. Na ni . . . kilianzia hospitalini, ama chochote kile, ama namna fulani ya jambo fulani ulilokuwa umefanya. Wala huwezi kulala, kinakusumbua sana. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, amini, nacho hakitakusumbua tena.

192 Mke wako ameketi hapo, huyo mama aliye karibu nawe aliyevaa nguo yenye mapambo ya madoadoa, ilimfurahisha sana, hata hakujua la kufanya. Hiyo ni kweli. Sikujui, mama, sivyo? Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Je, utanipokea kama nabii Wake? Kama nitakuambia, nasi hatufahamiani, kutoka hapa kwa kuwa wewe—wewe ni mwaminio, kwa sababu, ilimtokea, kama ukiniamini kwa moyo wako wote, nami naweza kukufunulia shida yako ni nini, utajua kama ni kweli au la. Sasa, wewe ni mgonjwa sana, ni ugonjwa wa moyo. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, amini kwa yote yaliyo ndani yako, nao utakuacha. "Usiogope; ni mimi; kuwa na moyo hodari."

193 Huyu hapa mama wa Kihindi, ameketi papo hapo nyuma akinitazama. Aliweka mkono wake juu kuzunguka kichwa chake, akisugua uso wake. Anasumbuliwa na matatizo mkononi mwake. Ee Mungu, jalia asiukose sasa. Dada Mhindi, ninazungumza nawe, Binti Jacobson, niamini kwa moyo wako wote. Hilo limempata. Haya basi. Amina.

194 Unaamini? Sasa, unaamini huyo ni Roho Mtakatifu? Inua mkono wako. Basi angalia, basi huo upako uko juu yangu sasa, na uniamini ninaposema ninasema kweli, naye Mungu anathibitisha kuwa ni kweli. Basi, Roho Mtakatifu yule yule, ila tu katika ofisi nyingine, yuko juu ya watu hawa, sisi sote. Sasa, tutasimama hapa juu, sisi sote tuliotiwa mafuta na Roho Mtakatifu, na kuacha kila mtu humu jengoni apite, nasi tutaomba na kuwawekea mikono. Nayo Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." "Zitafuatana *nao*," hiyo ni mimi na wewe pamoja, wewe pamoja nao. Unaona? Aminini. Tutawawekea mikono, na kuwaombea mnapopita. Tokeni kwenye jengo hili, mkishangilia na kufurahi tu, wala msiwahi kuiachilia, nanyi mtapata afya.

195 Sasa, kama mnaniamini mimi kuwa mtumishi wa kweli wa

Kristo. . .Nimezungumza nanyi kwa Neno la Mungu. Mungu ameshuka na kulithibitisha Neno la Mungu, nami nawajibu, nikiwaonyesha kwamba ni Mungu, nalo Neno la Mungu linaahidi hili kwa kila mmoja wenu. Anaweza kufanya nini cha zaidi? Hakuna. Yeye hawezi kuwaponya, maana Yeye tayari amefanya jambo hilo.

196 Kitu pekee ulicho nacho, cha kufanya ni kupitia papa hapa. Na mara tu unapoingia ndani ya maji na kubatizwa, unasema, "Mimi ni Mkristo, kwa sababu nimetubu na kubatizwa." Ukija hapa, na kuwekewa mikono, sema, "Nimeponywa, kwa maana Mungu alisema maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa huyo." Toka hapa, toka tu huku chini kana kwamba ulikuwa unatembea kutoka chini ya Kalvari, ukipaza sauti na kumsifu Mungu, imekwisha. Je, unaamini hilo? Amina! Ninampenda, nawe je? Amina.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Ambapo wenye dhambi wakitumbukia chini ya hayo mafuriko,
Hupoteza waa lao lote la dhambi.

Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahia kuiona
Chemichemi hiyo katika siku yake;
Hapo nijalie mimi, ingawa ni mwovu kama yeye,
Niliziosha dhambi zangu zote.

Tangu hapo kwa imani nilipokiona kile kijito
Kilichotoka kwenye majeraha Yako,
Upendo wa ukombozi umekuwa ndio wimbo wangu,
Na utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa.

Ndipo katika wimbo bora, mtamu zaidi,
Nitaimba uwezo Wake wa kuokoa,
Wakati maskini ulimi huu unaopiga kitembe, unaogugumiza
Utakapolala kimya kaburini.

197 Haleluya. Ninamwamini. Loo! Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa kila mmoja wetu. Loo, tunapotumbukia kwenye Mkondo huo wa uponyaji, unaomiminika kwa imani kutoka kwa Mungu Mbinguni, ukiwamiminia watu kuwaonyesha Uwepo Wake! Yeye yuko hapa sasa, anawapenda, anampenda kila mmoja wenu.

198 Ni wangapi wenu walio na kadi za maombi sasa? Inua mkono wako. Wale walio na kadi za maombi katika safu hii, sehemu hii, hebu wasimame kwenye ukuta upande ule, wote walio na kadi za maombi, simameni upande huo. Na wote walio na kadi za maombi katika sehemu hii, simameni kwenye marefu ya katikati. Na mara tu wanapofika mwisho, jongeeni moja kwa

moja hapa nyuma yao. Kisha mara kadi zote za maombi zikiisha, basi acha sehemu hii isimame upande huo. Nayo sehemu hii isiyo na kadi za maombi, wafuatane moja kwa moja. Ndugu Borders atashika kipaza sauti na kuwaelekeza.

199 Na sasa, njoni hapa ndugu zangu. Asante, Ndugu Eddie. [Ndugu mmoja anasema, "Kwako, Ndugu Branham ama kule chini?"—Mh.] Ni wapi tunapoweza kuwafikia vizuri zaidi? Huko chini? Nashangaa. . . ["Ngazi nyembamba."] Vema. Ndivyo. Huenda kuna baadhi yao ambao ni viwete. Nawaambia tutakalofanya, tutashuka huko. Hebu tushuke chini moja kwa moja, hilo ndilo tunaloweza kufanya, hivi sasa. Vema, njoni tu. Shukeni moja kwa moja, papa hapa chini, kila mmoja wenu enyi ndugu. Simameni tu hapo. . .?. . . [Sehemu tupu kwenye kanda.]

> . . . twonane! hata twonane!
> Hata twonane miguuni pa Yesu,
> Hata twonane! Hata twonane!
> Mungu awe nanyi daima!

200 Yeye si ni wa ajabu? Ni wangapi wanaamini kuwa utakuwa mzima na mwenye afya? Amina. Ni ajabu, ajabu jinsi gani! Mungu awabariki. Hebu tufumbe macho yetu sasa, tunapoachana, natumai kuwaona tena, na mpaka nitakapowaona nitakuwa nikiwaombea, muwe mkiniombea. Je, mtafanya hivyo? Sitasahau Port Alberni. Jambo pekee, laiti ningalikuwa na wakati zaidi wa kukaa; ninawapenda kwa upendo usiokufa wa Kikristo. Kamwe, wakati wowote ninapoweza kuwafadhili, usiku hautakuwa mrefu kupita kiasi, wala mvua haitanyesha kupita kiasi, nipigieni simu, nitawaombea wakati wowote, chochote ninachoweza kufanya nipate kuwa usaidizi kwenu, hata tutakapoonana tena.

> Hata twonane! Hata twonane!
> Mungu awe nanyi, hata tutakapoonana tena!

201 Wachungaji. Uvumisheni tu. Loo, ni ajabu jinsi gani! Ni vema jinsi gani ndugu kukaa pamoja kwa umoja, kama tu mafuta ya kupaka ya thamani, yaliyokuwa kwenye ndevu za Haruni, yaliyotiririka mpaka kwenye pindo za mavazi yake. Nachukia kuwaacha. Uh-huh. Mungu awabariki. Hebu tuuimbe tena, sivyo?

> . . . twonane! hata twonane!
> Hata twonane miguuni pa Yesu; (Hata twonane!)
> Hata twonane! hata twonane!
> Mungu awe nanyi. . .

Mungu akubariki, Ndugu.

62-0726 Ushuhuda Baharini
Legion Auditorium
Port Alberni, British Columbia Canada

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org